


**FODEN: SASA NAFURAHIA NAFASI NINAYOCHEZA**

UKURASA 22

**LISSU** na Kinana hapatoshi, Nape naye ajitosa

UKURASA 2



**WAZIRI** aliyejiuzulu ahojiwa na Kamati ya Maadili ya CCM

UKURASA 19

**SOKO** la mjini Moshi lateketea kwa moto usiku

UKURASA 19


# Nipashe

Jumatano Februari 7, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581579

www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper


# Mzigo bodaboda waielemea MOI

**WENGI** ni vijana, hawana bima wala fedha, idadi ya vifo; Zungu, Lema wanena yao... *Endelea ukurasa* 3

**Nusu ya wagonjwa wa MOI ni wa ajali za bodaboda**

**Dar, Morogoro, Arusha na Kilimanjaro hali mbaya**



**Kila nusu mwaka zinasababisha vifo 185 nchini**

**Wastani wa kumtibu majeruhi mmoja, milioni 2/- mezani**

## Bunge laanika mlolongo vikwazo shida ya umeme

UKURASA 2

## Tezi dume, kisukari sasa tishio

UKURASA 4

**MICHEZO** NIGERIA VS AFRIKA KUSINI, IVORY COAST VS DRC LEO UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Bunge laanika mlolongo vikwazo shida umeme

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, imeeleza sababu za uzalishaji wa umeme kuwa mdogo, hivyo kusababisha kukatika kwa umeme nchini.

Sababu hizo, kwa mujibu wa kamati hiyo ni upungufu wa maji kwenye mabwawa tegemeo ya Mtera, Kidatu na Kihansi, uchakavu wa mitambo, miundombinu ya kusafirishia umeme na upungufu wa gesi ya kuzalishia umeme.

Wakati kamati ikitaja sababu hizo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, amelieleza Bunge kwamba hadi kufikia jana, kulikuwa na upungufu wa megawati 193 kwenye gridi ya taifa.

Akiwasilisha bungeni, taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kuhusu shughuli za kamati kwa mwaka 2023, Mwenyekiti wa Kamati, Dk. David Mathayo, alisema upungufu wa umeme umefanya maeneo mengi ya nchi kuwa katika mgawo wa nishati hiyo.

Katika Bwawa la kufua umeme la Kihansi mkoani Morogoro, alisema kutokana na uhaba wa maji katika bwawa hilo, mtambo mmoja umezimwa, hivyo kuathiri uzalishaji wa umeme kwa kuwa hadi Septemba, mwaka jana, uzalishaji ulikuwa megawati 120.

Kutokana na hali hiyo, Bunge limeazimia serikali ihakikishe mradi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere (JNHPP), unakamilika haraka na kuanza uzalishaji kuanzia Februari, mwaka huu, kama ilivyoahidi.

Pia limeazimia serikali ihakikishe inafunga mitambo ya kupoza hewa katika Kituo cha Kinyerezi I Extention ili kuongeza uzalishaji kutoka Megawati 160 hadi 185 ifikapo Desemba, mwaka huu.

Pia limeazimia serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), iongeze uzalishaji wa gesi asilia katika visima vya Songosongo na Mnazi Bay (MB2 na MB3) ili kuongeza uzalishaji wa umeme.

Kadhalika, serikali ihakikishe mitambo ya kuzalisha umeme inafanyiwa ukarabati wa mara kwa mara ili kuepuka uchakavu ambao unaathiri uwezo wa mitambo hiyo.

Dk. Mathayo alisema taarifa iliyowasilishwa na serikali kwenye kamati katika vikao vya Januari, mwaka huu, ilionyesha hadi kufikia Desemba, mwaka jana, uwezo wa mitambo ya kufua umeme kutoka vyanzo mbalimbali vilivyounganishwa katika gridi ya taifa, ulifikia megawati 1,889.84. Kiasi hicho ni ongezeko la Megawati 195.29 katika kipindi cha mwaka mmoja, ikilinganishwa Megawati 1694.555 za mwaka 2022.

Alisema pamoja na ongezeko hilo, bado uzalishaji wa umeme nchini, ulikuwa wastani wa Megawati 1,200 kiasi ambacho ni kidogo kulinganisha na mahitaji ya Megawati 1,482.80, hivyo kusababisha upungufu wa wastani wa Megawati 283.

**KAULI YA BITEKO**

Akijibu hoja za kamati na michango ya wabunge, Dk. Biteko alikiri kwamba suala la kukatika katika kwa umeme linawakera wabunge, wananchi na Rais Samia Suluhu Hassan na hata wizara inakerwa nalo.

Alisema hakuna ubishi kwamba kama taifa linaweza kuwa na mipango mizuri ya kukabiliana na changamoto ya umeme, lakini serikali haijalala na imefanya juhudi kubwa. Alisisitiza kuwa walichoanza kuangalia ni mawanda mapana ya vyanzo vya kuzalisha umeme vina hali gani.

"Ninafurahi kusema kwamba baada ya mvua kunyesha, ukarabati wa mitambo, kuongeza gesi kwa maana ya mgandamizo wa gesi, upungufu huo umeendelea kupungua. Kwa leo (jana), tuna upungufu wa megawati 193 kwenye gridi ya taifa.

"Ni kweli kwamba mabwawa tuliyokuwa tunayatumia kwa ajili ya kuzalisha umeme yalikuwa yameshuka sana kiwango cha maji," alisema.

Kuhusu upungufu wa vituo vya kupoza umeme, Naibu Waziri Mkuu Biteko alisema kwa nchi nzima, vituo vinavyohitajika sasa ni 231, lakini vilivyopo ni 171.

# Lissu amvaa Kinana, kada Nape amjibu

**Na Elizabeth Zaya**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Bara, Tundu Lissu ameibuka kumjibu mwenzake mwenye cheo kama chake cha kisiasa kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana, akiwa na ufafanuzi uliobeba mchanganuo wa hoja ya CHADEMA kupokea fedha, akidai hazina kipya kwa kuwa ni haki yao.

Katika kile kinachoonekana kunoga kwa joto la siasa, Katibu Mwenezi wa zamani wa CCM, Nape Nnauye, ambaye sasa ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ndani ya saa baada ya tamko la Lissu, akajitokeza katika joho la kisiasa, akikosoa ufahamu wa kisheria wa Lissu na kile anachokitaja 'haki yao CHADEMA' si sahihi kwa sababu walipinga uchaguzi na stahiki yao ya ruzuku.

Tangu Kanali mstaafu Kinana Jumapili iliyopita atamke CHADEMA imepokea kimyakimya Sh. bilioni 2.7 za ruzuku, kumeibuka mlolongo wa majibizano kisiasa kati ya vyama hivyo, huku nje ya vyama nako hoja hizo zikitawala upepo wa siasa nchini, leo ikitimu siku nne.

Lissu, msomi wa sheria aliyeamua kumjibu Kinana, kigogo wa siasa, akitoa mchanganuo wa namna chama chao kilivyopata fedha hizo, chimbuko lake na uwanda mpana wa siasa unaoendana nao, huku akiorodhesha maeneo ya msuguano yanayozigusa pande hizo.

Lissu amesema majibu ambayo Kinana alipewa mwaka jana baada ya kutoa kauli kama hiyo kuhusu sababu ya mkwamo wa mazungumzo ya maridhiano baina ya pande hizo mbili ni kwamba wao hawahongeki na hawakuingia kwenye mazungumzo hayo kwa makubaliano ya kutoikosoa serikali pale inapokosea.

Lissu ametaja hoja za msingi za mazungumzo ya maridhiano hayo ni pamoja na kurejesha mchakato wa Katiba Mpya na kuboresha mfumo wa uchaguzi, zote zilikataliwa na CCM na ndiyo ikawa sababu ya mkwamo na si vinginevyo.

"Kwa taarifa yako, mazungumzo hayakuwahi kujadili chochote juu ya kauli, hatukuwahi kuzungumzia kwamba serikali inapokosea tusiikosoe, kilichokwamisha ni CCM kukataa Katiba na mfumo wa uchaguzi.

"Tuliwaandikia mapendekezo yetu na walipoyakataa waliandika kwa maandishi na majibu yalilenga kukataa hoja zetu tulizowapelekea tu na si hayo maneno mengine aliyoyataja Kinana kwamba ndiyo yalisababisha mazungumzo kukwama," Lissu alisema katika mazungumzo na mwandishi kwa simu jana.

"Kinana amesema CHADEMA hawana shukrani kwamba walikuwa na kesi kibao, tumewaachilia, badala ya kushukuru wanatutukana. Walitaka tuwashukuru kwa kutufutia kesi za uongo walizotufungulia, kututesa na kutuweka gerezani? Mwenyekiti wetu aliwekwa gerezani miezi minane bure. Kwahiyo, alipaswa apige magoti awashukuru hao waliomshtaki bure?" alihoji Lissu.

"Sisi hatuhongeki, kama mlifikiri mnatuachia kama hongo hiyo haipo, tutaendelea kusema pale tunapoona kuna makosa yanafanyika. Ukitufunga bure tutakusema na ukituachia bure tutakusema, na tutakusema mchana kweupe."

Kuhusu ruzuku ambayo Kinana alisema wameichukua kimyakimya, Lissu alisema katika mazungumzo yao, Kinana aliwahi kuwaambia ruzuku waliyostahili ilikuwa nyingi zaidi ya waliyolipwa.

"Kinana anasema eti ametupa ruzuku yetu, kama ni yetu ametupaje? Isingekuwa yetu angesema ametupa ruzuku isiyo yetu. Amesema ametupa yote, ni kweli kwa sababu ilikuwa yetu.

"Kinana huyohuyo na timu yake ametuambia sisi, si mara moja kwamba hiyo ruzuku tulikuwa hatuistahili, tulistahili nyingi zaidi. Sasa ruzuku ilikuwa ya kwetu au haikuwa ya kwetu... na kama haikuwa ya kwetu atuambie haikuwa ya kwetu," alisema.

Lissu alisema mpango wa chama hicho baada ya mkwamo wa mazungumzo hayo ya maridhiano yaliyolenga kutafuta mwafaka wa mambo ya msingi ikiwamo Katiba Mpya na kuwa na mfumo mzuri wa uchaguzi, watautafutia njia nyingine ikiwamo kupitia maandamano ya amani.

"Njia moja ikifungwa, kuna njia nyingine inafunguliwa, sisi tumeamua kutumia njia nyingine ya maandamano na tunaamini hiyo itasaidia," alisema Lissu.

**NAPE ALONGA**

Naye Nape alisema anaamini kwamba Lissu kama mwanasheria, anafahamu kile walichokipata kimetokana na maridhiano kwa sababu chama chao kilisema hakitambui uchaguzi.

"Kwanza sikutegemea CHADEMA na viongozi wake waende tofauti na walivyosema kwa sababu uwezo wao umeishia hapo. Lissu ni mwanasheria, anajua vizuri sana kwamba yale ambayo walikuwa wanayadai, na ambayo yaliingizwa kwenye maridhiano, pamoja na kwamba yeye anadai ilikuwa ni haki yao, bila maridhiano wasingeyapata.

"Kwa mfano, ruzuku ile inatokana na matokeo ya uchaguzi, CHADEMA walisema hawatambui uchaguzi na ndio maana usipoutambua uchaguzi, maana yake vile vinavyotokana na uchaguzi huna haki ya kuvipata, kwahiyo haikuwa haki yao."

Mbunge huyo wa Mtama alidai CHADEMA ilipofikia imegota na hakuna muujiza wa kuitoa ilipo.

Mwanzoni mwa mwaka jana, CHADEMA, CCM na serikali walianzisha mazungumzo ya maridhiano kuhusu mambo mbalimbali yaliyobeba hoja zaidi ya 10 ikiwamo mchakato wa Katiba Mpya, maridhiano ya kisiasa na Tume Huru ya Uchaguzi.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
Tarehe 06/02/2024

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe **07-02-2024** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **RUFIJI** mkoa wa **PWANI** kuelekea **DAR ES SALAAM,** gari hilo lenye namba za usajili:

**T 176 DFN / T 171 DFN.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | **-** | **mita** | **18.00** |
| **Upana** | **-** | **mita** | **2.80** |
| **Kimo** | **-** | **mita** | **5.00** |

3. Njia itakayotumika: Kutoka **RUFIJI** mkoa wa **PWANI** hadi **DAR ES SALAAM** kupitia **KIBITI - MLOKA ROAD.**

Gari itasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
07.02.2024

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa kuanzia siku ya **Jumamosi tarehe 10-02-2024** hadi tarehe **15-02-2024** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Taveta border** kuelekea **Kilombero kupitia Arusha, Manyara, Dodoma,** kupitia **Morogoro,** gari hizo zina namba za usajili: **T 853 DXS /T 887 DJB, T 453 DYG /T 837 DJB, T 478 ECF / T 393 DVS**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | **-** | **mita 22.00** |
| **Upana** | **-** | **mita 4.60** |
| **Kimo** | **-** | **mita 5.30** |

3. Njia itakayotumika: ***Arusha, Manyara, Dodoma, Morogoro*** hadi Kilombero gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

HABARI KITAIFA

# Bodaboda zinaua watu 31 kila mwezi

## ●MOI: Gharama zinatisha, wahusika hawamudu

**Na Restuta James**

USAFIRI wa pikipiki, maarufu bodaboda, umetajwa kugharimu uhai, kujeruhi na gharama za matibabu kwa wananchi wengi, huku Bunge likiitaka serikali kuwa na sheria itakayowapa adhabu kali madereva wa chombo hicho.

Imebainishwa kuwa asilimia 40 hadi 60 ya majeruhi wanaopokewa katika Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), wanatokana na ajali za bodaboda ambao takribani asilimia 80 hawana bima ya afya wala fedha za matibabu.

Aliyeibua kilio cha bodaboda kusababisha vifo na majeruhi ni Mbunge wa Shaurimoyo (CCM), Ali Juma Mohamed, ambaye juzi alitaka serikali iboreshe mfumo wa usafiri wa umma ili kuepuka matumizi ya usafiri usio rasmi.

Kutokana na hoja hiyo, Naibu Spika wa Bunge, Mussa Zungu, aliyekuwa akiongoza kikao bungeni, alisema usafiri wa bodaboda umekuwa kero mjini.

"Usafiri wa bodabora ni kero sana na hasa kwenye utumiaji wa sheria za barabara... mimi ni mtetezi mkubwa wa bodaboda, lakini matumizi yao ya barabara yanakatisha tamaa.

"Lazima (serikali) muwe na mkakati maalum wa kudhibiti ajali wanazozisababisha na lazima muwe na sheria kali za kuwadhibiti na hata kuwasimamisha, kwa sababu MOI ukienda sasa hivi asilimia 90 ni vijana," Zungu alionya.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, alibainisha kuwa taarifa ya MOI inaonesha kwamba kwa siku taasisi hiyo inapokea wagonjwa wa ajali 25 hadi 30. Kati yao, 13 wanatokana na ajali za bodaboda.

Mkuu wa Kitengo cha Utafiti MOI, Dk. Joel Bwemelo, alikiambia Kituo cha Televisheni cha Azam juzi kuwa asilimia 40 hadi 60 ya majeruhi wanaopokewa hospitalini huko wanatokana na ajali za bodaboda, wengi wakiwa ni vijana.

"Ajali za bodaboda zimekuwa nyingi, hata hao waliopata ajali ni vijana kuanzia miaka 16 hadi 45... asilimia 60 hadi 80 hawana bima, hivyo wakija hapa wao ni watanzania, ni lazima tuwatibu.

"Unakuta gharama halisi ya kumtibu huyo mgonjwa ni Sh. milioni mbili, lakini hana hata 60,000 ya kuchangia," alisema Dk. Bwemelo.

Alisema takwimu hizo zinashtusha na wanakusudia kukutana na wadau wa usafiri huo kuanzia wanaofundisha udereva, wanaowapima na kutoa leseni na Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), ili kuweka mikakati ya pamoja ya kuzuia ajali za bodaboda.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Kamishna Mwandamizi wa Polisi (SACP), Ramadhani Ng'anzi, alisema katika kipindi cha miezi sita, watu 185 wamepoteza maisha kwa ajali za bodaboda sawa na asilimia 21 ya vifo vya ajali 900 vilivyoripotiwa.

Hii ina maana kwamba kuna wastani wa vifo vya watu 31 kwa mwezi vitokanavyo na bodaboda nchini.

"Kwa majeruhi ajali za bodaboda zilichangia asilimia 13, mikakati yetu ni kuendelea kutoa elimu kwa kundi la bodaboda na katika marekebisho ya Sheria yetu ya Usalama Barabarani tunategemea kuongeza adhabu na faini za papo kwa hapo," alisema.

Mwishoni mwa mwaka jana, Sagini alisema asilimia 40 ya ajali zinazotokea nchini zinasababishwa na bodaboda na kulitaka kundi hilo kuzingatia Sheria ya Usalama Barabarani il kupunguza vifo na ajali zinazosababisha pia ulemavu wa kudumu.

Kwa mujibu wa takwimu za Jeshi la Polisi, mikoa inayoongoza kwa kuwa na pikipiki nyingi ni Dar es Salaam, Morogoro, Arusha na Kilimanjaro, ikiongoza pia kwa ajali za vyombo hivyo.

**KAULI YA LEMA**

Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema, alisema jana kuwa amefarijika kuona suala hilo linazungumzwa bungeni kwa kuwa alipotamka Machi mwaka jana kuwa bodaboda ni kazi ya laana, watu wengi hawakumwelewa.

"Hakuna siku imepita bila mimi kuona huruma kwa bodaboda kuanzia maisha yao na 'struggles' (utafutaji) zao. Ni kazi inayodhihirisha serikali kushindwa katika mipango yake ya uchumi na maisha ya watu. Pikipiki haipaswi wala haistahili kuwa usafiri wa umma.

"Watu waliofeli kuongoza ndio wanaweza kufikiri na kuona kuwa bodaboda ni ajira. Hii ni kazi inayozalisha umaskini wa kupindukia, maradhi, ajali, vilema, magonjwa na vifo vingi sana miongoni mwa kundi kubwa haswa la vijana. Ninarudia kusema tena kwa sauti kubwa kuendesha bodaboda ni umaskini mkubwa sana," alisema

Lema ambaye amewahi kuwa Mbunge wa Arusha Mjini (CHADEMA), alisema udereva wa bodaboda si kazi ya staha na ndio maana watoto wa viongozi hawawezi kuifanya na kamwe hawawezi kuwa na ndoto za kazi hiyo.

"Tuache siasa tuokoe maisha ya watu. Ni heri kukosa kura kuliko kulamba damu za watu kwa kushindwa kufanya uamuzi muhimu juu ya maisha yao. Tunaua kila siku na hatujioni kuwa na hatia," alisema.

# Watoa hoja nane kwa serikali kutokomeza ukeketaji nchini

**Na Sabato Kasika**

MTANDAO wa Kupinga Ukeketaji Tanzania, umetoa mapendekezo manane kwa serikali kwa lengo kutaka kusaidia kutokomeza vitendo hivyo kwa watoto wa kike na wanawake nchini.

Mkurugenzi wa shirika la C-SEMA, Michael Marwa, ambaye shirika lake ni miongoni mwa yanayounda mtandao huo, alitaja mapendekezo hayo kuwa ni kutungwa na kupitisha sheria ya kuzuia ukeketaji ili kulinda wanawake watu wazima wanaokeketwa.

Alikuwa anazungumza na waandishi wa habari katika ofisi za Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dar es Salaam jana kwenye maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukeketaji.

Marwa alisema wanapendekeza kurekebishwa kwa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kwa kuwa inachangia watoto kukeketwa na kuingizwa katika ndoa za utotoni na pia viongozi wa ngazi za juu kujitokeza wazi kuunga mkono jitihada zinazoendelea za kutokomeza ukeketaji.

"Lakini pia mtandao unashauri serikali kupitia wizara za kisekta kutenga bajeti ya utekelezaji mpango kazi wa kitaifa wa kutokomeza ukeketaji mwaka 2021 hadi 2024," alisema Marwa.

Marwa alitaja pendekezo lingine ni kutaka serikali itekeleze kwa vitendo mpango kazi wa kikanda wa nchi tano kuhusu ukeketaji unaovuka mipaka na pia isimamie kikamilifu ili watekelezaji vitendo hivyo wakamatwe na kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

"Tunatamani serikali idumishe ushirikiano na taasisi zisizo za kiserikali na mashirika rafiki ya kimataifa, ili kwa pamoja tuweze kutokomeza ukeketaji na ukandamizaji watoto wa kike na wanawake," alisema.

Katika pendekezo lingine, alisema jamii iungane na kukemea kwa nguvu vitendo vya ukeketaji na kutoa ushirikiano kwa vyombo vya dola, ikiwamo kutoa taarifa na ushahidi ili kufanikisha vita dhidi ya ukeketaji na ukatili wa kijinsia kwa ujumla.

Mtandao huo pia umependekeza wadau kuongeza juhudi katika kuzifikia jamii zinazotekeleza mila ya ukeketaji kwa elimu na kwa msaada wa moja kwa moja ili kutokomeza janga hilo.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa mwaka huu ni ukeketaji kwa kuwa unagawanyika kwa mbili, na kwamba serikali iweke mpango mkakati madhubiti na bajeti ya kutosha kusaidia wasichana wengi walio katika hatari ya kukeketwa.

Ofisa Programu wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), Neema Kasabuliro alisema pamoja na juhudi zinazofanywa na serikali, mashirika na taasisi mbalimbali, ukeketaji unaendelea kutekelezwa katika baadhi ya jamii.

"Kwa mujibu wa takwimu za Taarifa ya Demografia na Afya ya Mwaka 2022, ukeketaji unaendelea kupungua, lakini kwa kasi ndogo. Taarifa hiyo inasema asilimia nane ya wanawake wa umri wa miaka 15 hadi 49 wamekeketwa, umepungua kwa asilimia 10 kutoka takwimu za mwaka 2015 na 2016," alisema Neema.

Ofisa Mwandamizi, Jinsia, Wanawake, Watoto na Watu Wenye Ulemavu kutoka LHRC, Getrude Dyabene, alisema zipo juhudi kubwa zimefanyika katika wilaya mbalimbali ikiwamo mradi wa kutoa elimu na kusaidia watoto wa kike kukabiliana na mila ya ukeketaji.

"Mtandao unafanya kazi ya kuwezesha waathirika wa ukeketaji kufikia vyombo vya kisheria ikiwamo polisi na mahakama ili kuwachukulia hatua wale wote wanaoendeleza mila kandamizi," alisema Getrude.


VERRA Standards for a Sustainable Future

## MRADI WA TIST KUFANYA MKUTANO WA WAZI

Clean Air Action Corporation (CAAC) na Ukuzaji Maendeleo Endelevu Tanzania Limited (UMET) wanapenda kutangaza makusudio ya kufanya uthibitisho (validation) ya "Mradi wa TIST Tanzania VCS -011" (ID 4881) chini ya viwango vya Verra's Climate, Community and Biodiversity (CCB). Ni mradi wa miaka 60 ambao ulianza Tarehe 01-Januari-2000 utaendelea hadi 31 Desemba 2059. Kupata uthibitisho (validation), CAAC na UMET wanatakiwa waeleze pamoja na vitu vingine, kwamba TIST italeta manufaa kwenye mazingira, jamii na bionuwai (Viumbe na mazingira) yaani beneficial to climate, community and biodiversity. CAAC imewasilisha andiko la mradi (PD) kwa Verra (chombo kinachosimamia VCS na CCB.) na AENOR INTERNATIONAL S.A.U, CCBA ambaye ni mkaguzi aliyethibitishwa. Pia andiko la mradi limewasilishwa Kituo cha Usimamizi wa masuala ya Kaboni Tanzania, National Carbon Monitoring Center (NCMC) chombo kinachosimamia na kutoa taarifa juu ya kiasi cha kaboni na kuratibu michakato ya MRV kwa Serikali ya Tanzania.

Mradi unatarajia kupata cheti cha kiwango cha juu (gold level certification) katika nyanja zote tatu yaani mambo ya hali ya hewa, Jamii na Bionuwai (Climate, Community and Biodiversity). Mkutano wa wazi wa kukusanya maoni ya wadau utafanyika tarehe **12 Februari 2024, kuanzia saa 4:30 asubuhi mpaka saa 6:30** mchana kwenye ukumbi wa mikutano wa Chuo cha Biblia cha Anglikana Mt. Filipo Kongwa, Wilayani Kongwa Mkoa wa Dodoma, Tanzania. Katika kikao cha wadau maoni yatapokelewa. Tafadhali angalia kwenye tovuti iliyoandikwa hapo chini kusoma andiko la mradi. **https://registry.vera.org/app/projectDetail/VCS/4881**

Kipindi cha kukusanya maoni kwa verra kitaisha tarehe **22 Februari, 2024**

# Mbunge ataka mwongozo msamaha matibabu ya tezi dume na kisukari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Igalula (CCM), Venant Protas ametaka serikali kutoa mwongozo mahsusi wa msamaha wa matibabu kwa wagonjwa wa kisukari na tezi dume nchini, hasa wanaotoka familia maskini.

Akiuliza maswali bungeni jana, mbunge alisema wananchi maskini wamekuwa hawapewi msamaha na badala yake wamekuwa wanaulizwa maswali na kuambiwa wakatafute fedha za matibabu.

"Wizara kwanini isitoe mwongozo mahsusi ili wapate msamaha? Kwanini serikali isiweke ruzuku ya kukabiliana na magonjwa haya ili wananchi wapate matibabu ya uhakika?" mbunge huyo alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema Bima ya Afya kwa Wote itatatua suala hilo.

Alisema serikali inasisitiza utekelezaji Sera ya Afya ya Mwaka 2007 ya kutoa huduma ya msamaha kwa wananchi wasio na uwezo wa kulipia huduma za afya. Hata hivyo, wenye uwezo wa kulipia wataendelea kuchangia.

Alisema gharama ya kutibu wagonjwa wa kisukari kwa mwaka ni Sh. bilioni 300, na gharama za kutibu wagonjwa wote wa tezi dume ni Sh. bilioni 46.42, hivyo kupelekea jumla ya gharama za matibabu kwa magonjwa hayo kufikia Sh. bilioni 346.42 wakati bajeti ya dawa na vifaa tiba kwa mwaka ni Sh. bilioni 200.

"Hivyo, ikitokea huduma ya matibabu kwa magonjwa haya mawili kutolewa bure, itapelekea huduma nyingine katika nchi kusimama," alisema.

Naibu Waziri Mollel alibainisha kuwa kwa mwaka 2022/23, gharama ya msamaha wa matibabu kwa wagonjwa wa kisukari na saratani ya tezi dume ilikuwa Sh. bilioni 70.4.




Naibu Mkurugenzi Mkuu wa PanAfrican Energy Tanzania (PAET), Bizimana Ntuyabaliwe (kushoto), akichangia mada kuhusu "Miradi ya Umeme kwa Gesi ya Tanzania", wakati wa mdahalo wa mkutano wa Tanzania Energy Cooperation Summit 2024 (TECS), jijini Arusha mwishoni mwa wiki, uliolenga kuangazia fursa na vivutio kwa uwekezaji kwenye miradi ya gesi asilia nchini. PAET kwa kipindi cha miaka 20 sasa imekuwa ikichimba na kuchakata gesi asilia kutoka Songo Songo na kufikisha Dar es Salaam kwenye mitambo ya kuzalisha umeme na pia kusambaza kwa matumizi ya viwanda na katika mfumo wa Compressed Natural Gas (CNG) kwa matumizi ya magari. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makonda amwuliza DED 'kwanini usiandike barua kujiuzulu?'

## •Mwananchi aliyekatwa mapanga amliza

**Na Beatrice Shayo,** RUKWA

MKAZI wa Wilaya ya Sumbawanga, mkoani Rukwa, China Maharage, amemweleza Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, namna maofisa wa Jeshi la Uhamiaji wanavyofanya biashara haramu ya usafirishaji binadamu.

Hayo yalijiri juzi jioni wakati mwananchi huyo akitoa kero yake kwenye mkutano wa Makonda uliofanyika wilayani Sumbawanga ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake kwa ajili ya kukagua utekelezaji Ilani ya Uchaguzi na kutatua changamoto za wananchi.

Maharage alidai wapo maofisa wa Jeshi la Uhamiaji wanaoshirikiana na baadhi ya watu kufanya biashara hiyo na kuchukua fedha kwa wahamiaji haramu.

"Watu wanakufa kwenye magari, kuna ofisa uhamiaji hapa," alisema Maharage huku Makonda akimtaka amtaje kwa jina ofisa huyo.

"Anaitwa... (alitaja jina ambalo tunalihifadhi kwa sababu za kimaadili). Wanachua fedha kwa wakimbizi (wahamiaji haramu). Nikueleze namna wanavyochukua fedha, wanafanya hivi; wakishakamata wakimbizi wanawapeleka ofisini kwao, wanawachukua na kuwapeleka polisi, asubuhi kukicha wanawapeleka polisi wanaweza kutembea nao siku tatu hadi nne kwenda na kurudi nini kinachotafutwa, hapo ni namba," alisema Maharage.

Alisema inachukuliwa namba ya simu kwa wale wakimbizi wanakotoka, wanawatafuta ndugu zao ili watume fedha, zinaingia mikononi mwao na baada ya kuchukua fedha hizo wanawapeleka mahakamani na kuhukumiwa.

"Wamechukua Sh. milioni tano yakatolewa maelekezo wakimbizi waliotoa fedha zao za kujilipia faini mmekula ninyi mkawatoe saa tano usiku wakaenda gerezani kuwatoa na kukimbizwa Dar es Salaam," alidai.

Mwananchi huyo alisema kuwa kutokana na matukio hayo alikwenda kwa Kamishna wa Uhamiaji na kuongea na mbunge ambaye alimuunganisha na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alishindwa kukutana naye kwa kuwa hayuko vizuri kiuchumi.

"Nimekwenda Tunduma, kuna wakimbizi wanafungiwa ndani ya nyumba wakati kuna maofisa Uhamiaji. Kuna mwanamke mmoja anafanya kazi hiyo anawafungia ndani wanawapiga, kuwarekodi na kuwatumia picha ndugu zao wanatuma mamilioni ya fedha," alidai.

Maharage alisema fedha zikishatumwa wanawekwa kwenye malori na kuvushwa kwenda nchi jirani.

Mkazi wa Jimbo la Nsimbo, mkoani Katavi, Geofrey Mboje, alidai kukatwa mapanga akiwa anatetea haki za wenzake kwenye mgogoro wa ardhi na mpaka sasa Jeshi la Polisi halijachukua hatua.

Alidai Mkuu wa Wilaya ya Mpanda, Jamila Kimaro, baada ya kuwasikiliza, alitoa kibali kwa Mkurugenzi wa Halmashuari ya Nsimbo, Mohamed Ramadhani, kuwaruhusu wananchi hao kuendelea na shughuli zao.

Hata hivyo, alidai kuwa mkurugenzi huyo alilitoa eneo hilo kwa watu wengine bila kumjulisha Mkuu wa Wilaya na kusababisha wananchi hao walpofika katika eneo hilo kuvamiwa, kupigwa, baadhi kuuawa na wengine kujeruhiwa kwa mapanga.

Baada ya kumsikiliza, Makonda alimgeukia mkurugenzi, akisema "majeraha ya hawa watu na hao waliokufa inatokana na kauli zenu ninyi, ndio mliowaambia wakalime."

Mkurugenzi huyo alichukua kipazasauti na kukiri. Makonda aliendelea kumwuliza "hivi umenisikia vizuri lakini? Kwahiyo, hiki kipigo cha wananchi, kuuliwa na wengine kupata ulemavu ni matokeo ya kauli zenu?"

Mkurugenzi huyo alijibu kuwa "Mheshimiwa ni kweli waliruhusiwa kwenda kulima wananchi hao katika eneo hilo.

"Sasa unasubiri nini kuandika barua mwenyewe ya kujiuzulu? Yaani maumivu haya unaona faida gani katika utawala wako kichwa chake huyu kijana hakiwezi kurudi katika hali yake, ninyi bado mpo?" Makonda alihoji huku wananchi wakishangilia wakidai mkurugenzi ang'atuke.

"Mheshimiwa Makonda, nimekatwa mwili wangu mapanga 19, kichwani panga 13 na miguu mapanga sita. Nimevunjika mguu wakati nikitetea maslahi yetu.

"Ninajua umeagizwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kwa ajili ya kusimamia maslahi ya nchi hii. Kama kweli tunasema ukweli, viongozi wakubwa ndani ya mkoa huu wengi wao ni wabovu," alidai Mboje.

Alisema kinachomwumiza ni kwamba Jeshi la Polisi lipo, Mkuu wa Polisi Mkoa na Mkuu wa Upelelezi wapo lakini hakuna aliyekamatwa kushtakiwa kutokana na tukio hilo hadi sasa.

"Leo hii nimerudi nyumbani ninatishiwa amani, ninaambiwa watanimaliza, ninalindwa na watu zaidi ya 20 walio wema nyumbani kwangu kwa maana niliwatetea vyema katika ardhi hii," alidai.

Mboje alidai amekaa siku 30 hospitalini kupambania uhai wake na kumwomba Makonda amweleze Rais Samia namna anavyoteseka, wananyanyasika na wengine wanashindwa kuokoa maiti zao, watu wanazikwa mbugani na Jeshi la Polisi lipo.

"Hata mimi ninasema ni neema ya Mungu, ni Mungu alikuwa na mimi, nina shida ya kuonana na Rais Samia, usalama wangu ni mdogo. Ninaomba kuonana na Rais," alidai mwananchi huyo huku akilia.

Makonda baada ya kumsikiliza, alihoji viongozi wa eneo hilo, "huo ndio msaada mnaowapa wananchi wenu?"

Alisema tukio hilo limemwumiza na anashindwa kuendelea kuongea kwa kuwa anajisikia vibaya.

"Ninajisikia viabaya sana, ninaomba posho yangu yote nitamwachia, hili tukio lako nitakusaidia," alisema Makonda huku akitokwa machozi na kwenda kumkumbatia kijana huyo na kujikuta wote wanalia.

# TANGAZO

# NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| KIJITONYAMA | NEZAK INVESTMENT LTD | NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1019002 KIWANJA NAMBA P23439 KIFURU-KINYEREZI | ZACHARIA ANTHONY KAPAMA | KIFURU KINYEREZI-ILALA | 14/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | WAWA COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 115345, KIWANJA NAMBA 124, KITALU '24' KIBADA KIGAMBONI 2.NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1002975 KIWANJA NA. 2483, KITALU 'A' MBEZI MANYEMA 3.NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.KND/KGG/KATI/214 KIGOGO KATI 4. NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOPO KINZUDI GOBA | 1.SALUM JUMA NYANDOTO 2. SALUMU JUMA NYANDOTO 3.SALUM JUMA MARWA 4.SALUMU JUMA NYANDOTO | 1.KIBADA- KIGAMBONI 2.MBEZI MANYEMA 3.KIGOGO KATI 4.KINZUDI GOBA | 15/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MAIN | TOMONI FARMS LIMITED | SHAMBA LENYE HATI YA MAUZIANO YA SERIKALI YA KIJIJI, EKARI 194 | FRANKLIN G. BAGALLA | KIJIJI CHA TOMONI-KIBITI RUFIJI | 16/02/2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | LUCAS NTIRUHUNGWA MZYENGE | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JAFETH YONA MZAVA | MIKWAMBE- KIGAMBONI | 21/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | HP PLANNERS & EVENTS MANAGEMENT | NYUMBA (2) | 1.JAMES NDASKOI NNKO 2.DAPHROSER ABEID HAMZA | 1.TEGETA 2.KIGAMBONI | 16/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | FELIX BIRCKMAS ALOYS | NYUMBA (2) | 1.KASSIAN ANTHON NINDI 2.BOSCO ULIRICK TARIMO | 1.TABATA KISUKULU 2.MANZESE | 21/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | RAYSONS AND COMPANY | NYUMBA | RAYMOND MICHAEL MREMI | KIBAHA | 16/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | GRACE ADONIAS MTEGO | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.22 KITALU 'N' HATI NA.4870 | BLASIUS SWAI KAGINA | BUNDA | 14/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | ABAS HAMAD ISSA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PETER NDULU MAHARAGE | MISUNGWI-MWANZA | 16/02/2024 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARIA JOHN PETRO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JOHN PETRO KALISA | KILOLELI 'B' - MWANZA | 20/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.NYUMBA 2. KIWANJA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.IGELEGELE BUGARIKA 2. BUJINGWA-MWANZA | 16/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | SELEMANI CHARLES MNIKO | NYUMBA | SELEMANI CHARLES MNIKO | MBUGANI -MWANZA | 19/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JAMES JACOB KALULEMA | NYUMBA | JAMES JACOB KALULEMA | MAHINA KANYERERE-MWANZA | 20/02/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | CHACHA ITEMBE NYAMAISA | NYUMBA | SHAABAN SHILLINDE BULILO | NYAMHONGOLO | 19/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | NCHAMA SKANIA MANGORYO | NYUMBA | NCHAMA SKANIA MANGORYO | MKOLANI MWANZA CITY | 22/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | ALOYCE ALOYCE KIMARO | NYUMBA | YAHAYA HUSSEIN ATHUMAN | PASIANSI MWANZA | 19/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARIANA BENEDICT MASSAWE | NYUMBA | SHIJA DAUDI NDUNGILE | ZENZE - ILEMELA | 23/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | SIKITU HAMIS YAHAYA | NYUMBA | HAJI ABEID KASUBI | NYASAKA ILEMELA MWANZA | 19/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | SUNNY KEWAL SINGH | NYUMBA | BERNARD PATRICK MABINZA | MBEZI MSAKUZI | 21/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | DENIS SASITA KAPONGO | NYUMBA | SAID JUMA KHAMISI | KIBWAGOGO -ZINGA BAGAMOYO | 23/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | MSHAMU MOLELI MAPUNDA | NYUMBA | MSHAMU MOLELI MAPUNDA | MIKWAMBE -TUANGOMA | 27/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | MATHAYO GABRIEL MJEMA | NYUMBA | MATHAYO GABRIEL MJEMA | TEGETA-MIVUMONI | 15/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | HAFIDH HASSAN HAFIZO | NYUMBA | HAFIDH HASSAN HAFIZO | MWANDEGE- MKURANGA | 28/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | ZULFA SALIM SALUM | NYUMBA | HILAL MATHIAS MAPUNDA | MAJI MATITU-MBAGALA | 14/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| HEAD OFFICE | FLORIAN CLAVERY RUGEMALIRA | GARI BMW X5 GH-FA30N | FLORIAN LUGEMALIRA CLAVERY | ARUSHA | 13/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | LAMECK RICHARD RWEYONGEZA | NYUMBA | LAMECK RICHARD RWEYONGEZA | KIVULE | 21/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | MASUDI JUMANNE RAMADHANI | NYUMBA | BEATRICE STEPHANO KISHERU | SARANGA | 27/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | NASSOR KHALID OTHMAN | NYUMBA | BAHATI SUMBU MTINDYA | MBEZI MAKABE | 27/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | VICTOR STEVEN MANG'ANA | NYUMBA | VICTOR STEVEN MANG'ANA | UKONGA | 21/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | HASSAN RAMADHANI SHEKIKA | NYUMBA (2) | 1.HASSAN RAMADHANI HARASHI 2.HASSAN RAMADHANI SHEKIKA | 1.YOMBO DOVYA-MAKANGARAWE 2.TAMBANI MKURANGA | 15/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | MHINA JOSEPH KWELLA | NYUMBA | MHINA JOSEPH KWELLA | PUGU | 20/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | INNOCENT DIDAS MUMBURI | NYUMBA | KHADIJA SEIF SINKAMBA | VINGUNGUTI- ILALA | 21/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | KOKUBELWA PAUL NGAMBEKI | KIWANJA | ANTHONY AARON ICHWEKELEZA | MPIJI MAGOE | 15/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | OWDEN MKUMBALA NYONDO | NYUMBA | OWDEN MKUMBALA NYONDO | ISYESYE-MBEYA | 20/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | WILLY MWITIKA MGOGO | NYUMBA | WILLY MWITIKA MGOGO | MLOWO-MBEYA | 16/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | ALFRED MICHAEL PANGANI | NYUMBA | ALFRED MICHAEL PANGANI | SHEWA -MWAKIBETE | 21/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 21/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA ZENYE HATI YA MAUZIANO | FRENK SAMSON LEMAU | SHEWA-MBEYA | 22/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | MERY STANLEY MOSHA | NYUMBA | MERY STANLEY MOSHA | LUGURUNI-UBUNGO | 23/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | JENIPHER SILVESTRY KIMARO | NYUMBA (2) | 1.JENIPHER SILVESTRY KIMARO 2.GERALD ABIMELECK SHOO | 1.MSINGWA KATA SARANGA 2. KEREGE-BAGAMOYO | 28/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | ZARINA SHAMTE MADABIDA | NYUMBA | ZARINA SHAMTE MADABIDA | VIKAWE KIBAHA | 21/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | MARIAM ADINAN MCHARO | NYUMBA | MARIAM ADINAN MCHARO | NYAKASANGWE WAZO | 22/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | FOCUS JOSEPH KICHINDA | NYUMBA | FOCUS JOSEPH KICHINDA | MJI MPYA-KIMARA | 23/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGEA | DEODATUS RWEHANGULA MGURUBI | NYUMBA | DEODATUS RWEHANGULA MGURUB | BUNJU | 22/02/2024 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | SHAMTE ATHUMANI JONGO | NYUMBA | JOSEPH MERKIORY PETER | CHAMAZI DOVYA | 26/02/2024 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | FATUMA BAKARI BENDERA | NYUMBA | FATUMA BAKARI BENDERA | KIMELE-VIKAWE | 21/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | JUMBE MHINA SALUM | NYUMBA | JUMBE MHINA SALUM | MKENGE-VIKAWE | 21/02/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | PADONI KIBAYU SIMON | NYUMBA | PADONI KIBAYU SIMON | MAJOE-VIWEGE | 27/02/2024 SAA 06:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| TEGETA | SALUM SULEIMAN MWANYIRO | NYUMBA | SALUM SULEIMAN MWANYIRO | BUNJU 'B' | 22/02/2024 SAA 06:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| TANDALE | EWALD EDWARD TEMBA | NYUMBA | TATU MOHAMED NGARONGA | JONGO-MAKURUMLA | 28/02/2024 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MKONDA HOUSE OF FOOD | NYUMBA | PAMELA MACHIRA NYITAMBE | TABATA-KIMANGA | 27/02/2024 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | CESILIA SAMWELY KWEKA | NYUMBA | LEONARD JACOB NUBWA | MBAGALA | 26/02/2024 SAA 06:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| UBUNGO | LISTER BENEDICT CHIMYA | NYUMBA | LISTER BENEDICT CHIMYA | KIMARA KING'ONG'O | 23/02/2024 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | MARY MEDARD SILAYO | NYUMBA | MARY MEDARD SILAYO | KIBAMBA-MLOGANZILA | 23/02/2024 SAA 07:00 MCHANA NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0715868000/0714939933/0785242219/0759282344/0787129539/0767808848/0754497396/0678799566/0655715138
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

**MAONI & UCHAMBUZI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Muhimu kushirikiana kudhibiti mmomonyoko maadili

**KATIKA** maadhimisho ya wiki ya sheria maeneo mbali mbali nchini, kumeibuka suala la watu kutoelewa elimu ya sheria na kutambua haki yao pale linapojitokeza suala linalohitaji msaada wa kisheria.

Pia, kuna matukio yanayoendelea kufanyika, lakini kwa kuwa jamii haielewi nini cha kufanya, matukio hayo yanaendelea kufanyika na kusababisha madhara kwa wale wanaotendewa.

Kuna suala ambalo kwa sasa limekuwa tishio kubwa hasa kwa wanafunzi wavulana linalojitokeza katika shule mbalimbali la watoto kuingiliana kinyume na maumbile.

Shule hizo zinajulikana na kutajwa kuwa vinara katika vitendo hivyo, lakini kinachoshangaza vinaachwa vikiendelea bila juhudi za kuvikomesha kutotiliwa umuhimu.

Suala hilo huja kuibuka kama kiongozi ataitembelea shule hiyo na ndipo wazazi hutoa malalamiko baada ya kugundua watoto wao wakiwa wanaharibika.

Vitendo hivi vya mmomonyoko wa maadili vinaonekana kushamiri hasa katika shule kuanzia za msingi hadi sekondari.

Vinafanyika huko kwa sababu watoto ni rahisi kurubuniwa na kuingia kwenye mtego huo na matokeo yake taifa baadaye kuwa na watu wasiofaa.

Viongozi wa dini mbali mbali wamekuwa wakikemea vitendo hivi vya mmomonyoko wa maadili kwa sababu sio vya kumpendeza Mungu.

Hata kwenye maandiko matakatifu vinakatazwa kwa kuwa vinasababisha laana na kukuta taifa likiangamia.

Umuhimu wa kushirikiana kudhibiti vitendo hivi ni mkubwa kwa kuwa bila umoja, nguvu ya kudhibiti itakuwa ndogo na vitaendelea kufanyika.

Inasikitisha kupata taarifa ya shule ya msingi kutajwa kushamiri kwa vitendo vya wanafunzi kuingiliana kinyume na maumbile.

Hii tabia mtu anaweza kujiuliza mzizi wake umetokea wapi mpaka kuwa kinara na je walimu wanatambua kuwapo kwa suala hilo na hatua gani zinachukuliwa.

Vilevile kwa wazazi na walezi wa watoto hao, je wana muda wa kuongea na watoto wao kujua maendeleo ya watoto wao na changamoto wanazopitia wanapokuwa shuleni na hata wanaporudi nyumbani kwenye njia wanazopita.

Ndio maana suala hilo linahitaji ushirikiano wa hali ya juu kutoka kwa wazazi na walimu pamoja na serikali ili kulidhibiti na kuliepusha taifa katika janga la kuwa na watu wasiokuwa na manufaa katika uzalishaji.

Nchi yoyote ili iendelee ni lazima iwe na nguvukazi ya watu, kama kizazi cha sasa kitaharibiwa nguvukazi itatoka wapi? Watu watashindwa kuzaana na matokeo yake nguvukazi ya kuleta maendeleo ya nchi itapotea.

Suala hili linahusu watu wote kila wanapoona vitendo hivyo vikifanyika kuchukua hatua mara moja ili kudhibiti.


Imeelezwa kuwa kuna ambao tayari wameshakamatwa kwa kuhusika na vitendo hivyo na wengine kesi zao ziko mahakamani, ni vyema pia wananchi wakatoa ushirikiano kwa kutoa ushahidi mahakamani ili sheria iweze kuchukua mkondo wake.

Mara nyingi linapojitokeza suala la watu kujitokeza kutoa ushirikiano mahakamani huwa tatizo, hawajitokezi na matokeo yake ushahidi kukosekana na aliyefanya kosa hilo kuachiwa huru na kuendelea kulifanya zaidi mitaani kwa kuharibu watoto kimwili na kisaikolojia.

Umuhimu wa watu kutambua kuwa jambo fulani ni kosa ni kitu cha msingi kwa kuwa hiyo ndio njia ya kuwawezesha kutoa taarifa kila wanapobaini tatizo.

Wiki hii ya sheria itumike vyema kutoa elimu kwa jamii kutambua haki zao za msingi za kuripoti taarifa za vitendo vibaya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




**Muungwana Lazima Nilonge**

Na Mwandishi Wetu

# Juhudi ni muhimu kutokomeza ukoma

**KUNA** imani inayoendelea kujengeka kwenye jamii kuwa ukoma umetokomezwa Tanzania.

Inawezekana siyo sahihi ukoma upo. Japo si kwa kiasi kikubwa kama ilivyokuwa zamani ambako kulikuwa na vituo vya kuhudumia watu wenye maradhi hayo kimojawapo kikiwa Kindwiti kilichoko Rufiji mkoa wa Pwani.

Lakini licha ya kupungua watu huuhusisha na imani potofu inayotokana na baadhi ya kushindwa kufahamu dalili zake na wengine wakiuhusisha ukoma na ushirikina au magonjwa ya kurithi.

Dhana hiyo potofu imejengeka miongoni mwa jamii kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukosa elimu ya ugonjwa huo na dalili zake.

Ugonjwa huu unaambukizwa kwa njia ya hewa kama ilivyo kifua kikuu ni baada ya mwenye maambukizi kuueneza kwa kupiga chafya, kukohoa, kuongea au kucheka.

Miaka ya nyuma kulikuwa na dhana kuwa ugonjwa huo unaambukizwa kwa njia ya kugusana, licha ya kwamba hapo awali ilidhaniwa hivyo lakini tafiti zimethibitisha kuwa husambaa kwa njia ya hewa na si kwa kugusana.

Maradhi haya husababishwa na bakteria au vimelea jamii moja na wale wa kifua kikuu wajulikanao kama 'mycobacterium Leprae (M.Leprae).

Wataalamu wa afya wanataja dalili za ukoma kuwa ni mabaka ambayo hayawashi wala hayana hisia katika ngozi na mishipa ya fahamu kuvimba.

Aidha, wanasema kuwa mtu ambaye ana mabaka matano huo ni ukoma hafifu na mwenye mabaka zaidi ya matano ni ukoma mkali na kuwashauri kuwahi hospitalini kwa matibabu.

Katika jamii kuna watu wanapokuwa na dalili hizo za ukoma wanaamini kuwa wamerogwa na kukimbilia kwa waganga kupiga ramli na hata kupata tiba kwa kutumia dawa za miti shamba, bila mafanikio.

Wengine wanaamini kuwa ukoma ni wa kurithi kutoka kwa mababu na wazazi na kushauri kuwa njia pekee ni kwenda kufanyiwa matambiko kwenye mizimu ili usitokee kwenye vizazi vijavyo na ukoo wao.

Wapo wanaoamini kuwa dalili hizo za ukoma ni mchafuko wa damu mwilini, fangusi na minyoo, hivyo kuamua kuanza kujipatia tiba kiholela kwenye maduka ya dawa baridi bila ya kuonana na madaktari na kufanya vipimo.

Tanzania bila ya ukoma na magonjwa mengine, inawezekana, iwapo jamii itazingatia ushauri wa wataalamu wa afya wa kuyadhibiti kwa kushirikiana na serikali na wadau wengine.

Kama watu wanataka jamii iliyo salama, kwa pamoja wanalazimika kubadilika na kuachana na mila na desturi au kuishi kizamani na kuamini ushirikina.

Wataalamu wa afya wanapaswa kuwafuata walioathirika majumbani na kufanya utafiti badala ya kuwasubiri hospitalini ili kuibua wagonjwa kama wanavyofanya kwa wafikia wenye kifua kikuu.

Lakini pia jamii ifahamu ugonjwa huo na dalili zake ili wagonjwa wafikishwe hospitalini mapema kupata tiba na kudhibiti maambukizi na kuwaepusha wengine.

Ikumbukwe mikoa yenye wagonjwa wa ukoma ni pamoja na Morogoro, Lindi, Tanga, Katavi, Dar es Saalam, Geita, Tabora, Dodoma, Mtwara na Ruvuma.

Ni vyema juhudi zikafanyika zaidi na kuboresha huduma za afya kwa wananchi ili kupunguza magonjwa hayo ambayo yanaharibu viungo vya nguvu kazi na kusababisha ulemavu.

Ukoma unaambukiza kwa njia ya hewa, hivyo wananchi waelimishwe kuepuka kukaa kwenye msongamano na kujenga nyumba zenye madirisha makubwa kwa ajili ya kupitisha hewa ya kutosha.

Lakini pia kuachana na kuuhusisha ukoma na imani za kishirikina ama kuwa ni wa kurithi jambo ambalo siyo sahihi kwa mujibu wa wataalamu.

Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha kuwa ukoma umepungua nchini na kuna mikoa ambayo kwa kipindi cha takribani miaka mitano haijaripotiwa kuwa na ugonjwa huo.

## Serikali yasaka dawa ya uhaba wa walimu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

SERIKALI imeanza majaribio ya mfumo wa ufundishaji mbashara ambao mwalimu mmoja anaweza kufundisha wanafunzi zaidi ya 1,000 kwa wakati mmoja.

Mfumo huo ambao kwa sasa unafanyiwa majaribio kwa baadhi ya shule za mikoa miwili ya Pwani na Dodoma, unamwezesha mwalimu kutoka kituo kimoja kufundisha wanafunzi wengi kwa wakati mmoja wakiwa mikoa tofauti.

Utaratibu huo unaleta tafsiri ya kwamba mbali na kurahisisha utendaji kazi, pia ni njia mojawapo ya kukabiliana na uhaba wa walimu, hasa wa masomo ya sayansi shuleni.

Wakati serikali inaendelea na majaribio ya mfumo huo, wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kibaha wamesema mfumo huo utawasaidia kupata uelewa kwa wepesi na kufanya vizuri kwenye mitihani ya kitaifa.

Wametaja faida nyigine kuwa ni pamoja na kuokoa muda, jambo ambalo litawezesha kukamilisha mada zote kwa wakati.

Mmoja wa wanafunzi hao, Elihuruma Thomas alisema jana kuwa ni teknolojia nzuri ambayo inaweza kuwa mwarobaini wa kukabiliana na uhaba wa walimu hususani wa masomo ya sayansi.

"Mfumo huu utakapoanza kikamilifu utaleta faraja kwa wanafunzi kwa kuwa tutakuwa tunakamilisha mada za masomo mapema na kisha kuanza marudio ya masomo, hivyo itatuwezesha kufanya vizuri kwenye mitihani ya taifa," alisema Zaharuki Hamisi.

Mkufunzi wa ujuzi wa namna ya kutumia mfumo huo kwa walimu, Jackson Mhoro ambaye ni Mtaalamu wa TEHAMA kutoka Shirika la Elimu Kibaha, alisema mpaka sasa walimu wanne kutoka shule hiyo wameshapata ujuzi huo na wengine wanendelea kujinoa, lengo likiwa kuwafikia wote.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Kibaha, George Kazi, alisema ili kwenda na wakati katika matumizi ya mfumo huo, tayari wameandaa maudhui ya masomo ambayo hivi sasa yako kwenye hatua ya kufanyiwa maboresho.

Ofisa Elimu Mkoa wa Pwani, Sara Mlaki alisema matumizi ya mfumo huo yatarahisisha ufundishaji na kuongeza ufaulu kwa wanafunzi na kwamba hivi sasa hatua inayofuata ni kuboresha miundombinu ya madarasa ili iendane na mahitaji ya mfumo huo.

# Madiwani wavutana michango ujenzi shule maalum ya mkoa

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma limeazimia kumwandikia barua Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma kumwomba abadilishe utaratibu wa halmashauri yao kuchangia ujenzi wa Shule ya Wasichana ya Mkoa huo inayojengwa katika Halmashauri ya Madaba.

Maazimio hayo yametolewa baada ya kuibuka mvutano mkubwa miongoni mwa madiwani, wakipinga maelekezo ya awali ya kuitaka halmashauri yao kuchangia Sh. saba kwa kila kilo moja ya mazao yatakayouzwa kupitia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani.

Baadhi ya madiwani hao walisema makato hayo kulingana na maelekezo hayo yataifanya halmashauri yao kuchangia kiasi kikubwa mno kulinganishwa na halmashauri zingine ambazo hazina mazao yanayouzwa kupitia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani.Walisema Tunduru inauza korosho, ufuta na mbaazi kupitia mfumo huo, hivyo uongozi wa mkoa kama utaendelea na msimamo huo, shule hiyo ni dhahiri itajengwa kwa asilimia kubwa na Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ilhali wao pia wanayo matatizo mengi yanayotakiwa kutatuliwa kupitia fedha za makusanyo toka mauzo ya mazao.

"Sisi hatupingani na maelekezo ya ujenzi wa shule, bali tunaomba viongozi wa mkoa kutengeneza bajeti na kuigawa kwenye halmashauri zote kwa kiwango sawa ili shule hiyo ijengwe kwa kiwango sawa cha michango kutoka katika halmashauri zote," alisisitiza Diwani wa Namiungo, Salima Limbalambala, akiungwa mkono na Diwani wa Viti Maalumu Tarafa ya Matemanga, Stawa Timamu.

Madiwani hao walisema mkoa unafikiria kujenga Shule ya Wasichana katika Halmashauri ya Madaba ambako ni Km 400 kutoka Tunduru ilhali Wilaya ya Tunduru iko nyuma katika maendeleo ya elimu.

Walitolea mfano upungufu wa mabweni katika shule zao, hali ambayo imesababisha wanafunzi wa kike kupanga kwenye nyumba za wananchi na huku 614 wakipata ujauzito utotoni na kushindwa kuendelea na masomo.

Madiwani hao walisema uongozi wa mkoa ulitakiwa ulione hilo kuwa ni tatizo kwa wilaya hiyo na kuonesha hali ya huruma kwa kuruhusu shule hiyo kujengwa Tunduru badala ya Madaba.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Said Bwanali alisema fedha hizo zilizoelekezwa kutoka kwenye mauzo ya mazao ni nyingi, hivyo akataka busara itumike pasi kuathiri mipango na maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Ushauri wa Maendeleo Mkoa (RCC).

Alisema jambo hilo hivi sasa limeanza kutumiwa na wanasiasa kuwashauri wananchi kugomea shughuli za maendeleo, hivyo linaweza kuwasumbua kipindi cha uchaguzi.




Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba (kulia) akimkabidhi taarifa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, baada ya kumaliza kikao baina ya NSSF na TAA jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## RC Makalla aikaribisha NSSF kuwekeza uwanja wa ndege

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, ametangaza fursa mbalimbali zilizoko katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza huku akialika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kuwa mbia muhimu wa uwekezaji kwenye uwanja huo.

Kiongozi huyo aliyasema hayo juzi wakati wa kikao na Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), Mussa Mbura, kilichofanyika Makao Makuu ya NSSF jijini Dar es Salaam.

Alizitaja fursa za uwekezaji katika uwanja huo kuwa ni kuendeleza uwanja huo kwa kuboresha jengo la abiria lililopo, pia kujenga jengo kubwa la abiria ambalo litakuwa na hadhi ya kimataifa, kuboresha njia ya kutua na kuruka ndege, kuboresha mfumo wa taa za kuongoza ndege pamoja na kujenga hoteli ya kitalii yenye hadhi ya nyota tano.

Makalla alishukuru mfuko huo kwa kuonesha nia hiyo pamoja na TAA kwa kuwa tayari kukaribisha NSSF katika uwekezaji na kuona utayari wa taasisi hizo mbili za serikali kufanya kazi kwa pamoja ili kukuza uchumi na kuleta maendeleo.

"Tunawakaribisha wadau wengine. Kwa sasa kipaumbele tumeanza na NSSF kwa sababu tayari wameshawekeza katika mradi wa jengo la hoteli ya nyota tano na sisi Mkoa wa Mwanza tunawashukuru kwa sababu tuna mkakati wa kukuza utalii katika jiji letu.

"Pamoja na mambo mengine, NSSF tayari wameonesha nia ya dhati ya kuendelea kuwekeza katika Mkoa wa Mwanza," alisema Makalla.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Mshomba, alimshukuru Makalla kwa kuwa na kikao na taasisi hizo ambacho kilitumika kuzungumzia mambo mbalimbali ikiwamo kutoa kipaumbele kwa NSSF kuwa mwekezaji mkuu katika kuendeleza Uwanja wa Ndege Mwanza.

"Tunaendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo ameendelea kufungua nchi na kutuletea fursa za wawekezaji ambao kwetu sekta binafsi ni sekta muhimu kwa kuandikisha wanachama na kukusanya michango," alisema Mshomba.

Alisema NSSF kwa kushirikiana na TAA watafikia hatua ya makubaliano na hatimaye waendelee katika hatua ya utekelezaji kwa maeneo ambayo wameyabainisha ambayo yataleta faida katika uwekezaji mradi huo kwa kuwa lengo ni kujenga uchumi wa nchi.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TAA, Mbura, alisema mamlaka hiyo imewasilisha fursa mbalimbali kwa NSSF ili washirikiane kuwekeza katika Uwanja wa Ndege Mwanza.

Alisema TAA pia inamshukuru Rais Samia kwa kuiagiza kufanya maboresho katika uwanja huo. Tayari fedha kwa ajili ya maboresho hayo zimeshafika na hivi punde wataanza ukarabati wa jengo hilo.

Mkoa wa Mwanza ni miongoni mwa mikoa ambayo iko karibu na mbuga za wanyama, ikiwamo mbuga kubwa zaidi Serengeti, kupitia Mwanza ambapo inamchukua mtalii saa moja awe ametoka nje ya nchi au ndani ya nchi na kwenda Serengeti kutalii na kurudi Mwanza.

Mwanza pia ni moja ya mikoa nchini ambayo ina shughuli nyingi za kiuchumi ikiwamo uvuvi, kilimo, uchimbaji madini, utalii na biashara, hivyo kuwa na mzunguko mkubwa wa watu na kupelekea Uwanja wa Ndege Mwanza kuwa na watumiaji wengi.

# Mahakama yatoa uamuzi mirathi iliyozua mvutano

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Mwanzo Nzega imemaliza kufanya usuluhishi kwa familia inayovutana kusimamia mirathi ya Zena Shemshadini ambaye hakuacha watoto, mume, wazazi wala wajukuu na imeamuru aliyeteuliwa kusimamia akusanye mali za marehemu.

Uamuzi huo wa mahakama ulifikiwa katika usuluhishi mbele ya Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Abunas Sonyo ambapo wanafamilia waligawanyika, kila upande ukitaka kusimamia mirathi hiyo.

Salma Mohammed alifungua shauri akiomba kusimamia mirathi hiyo wakati tayari Mahakama ilishamteua Karim Samji kusimamia. Wakati Mahakama hiyo inatoa uamuzi wa kumteua msimamizi wa mirathi, hakukuwa na pingamizi kutoka kwa wanafamilia, lakini baada ya uteuzi aliibuka Salma ambaye ni mtoto wa mdogo wa marehemu, akafungua shauri akiomba kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi.

Baada ya mahakama kuona mvutano huo, iliamuru pande hizo mbili kuingia kwenye usuluhishi na baada ya kumalizika, iliamuru msimamizi aliyeteuliwa awali kuendelea kusimamia mirathi.

Hakimu Sonyo alisema msimamizi wa mirathi anatakiwa kukusanya mali za marehemu, kuwasilisha orodha ya mali hizo na mgawo mahakamani Februari 13, mwaka huu.

"Tunafikia mwisho, msimamizi wa mirathi alete orodha ya mali na mgawo. Kama hakutakuwa na pingamizi, mchakato utakuwa umemalizika, waendelee na hatua nyingine ya kupeleka Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kupata hati ya nyumba iliyopo kwenye mirathi," alisema Hakimu Sonyo.

Awali Samji aliwasilisha kiapo mahakamani, akidai marehemu ni mama yake mdogo, amefariki dunia akiwa hana watoto, mume, wazazi wala wajukuu. Watoto waliopo ni wa dada zake na mwombaji ndiye mtoto pekee.

Alidai marehemu hakuacha wosia na maelezo hayo yaliungwa mkono na wajukuu Gullam Siager na Haji Seager, hivyo mahakama ikamteua kusimamia mirathi hiyo.

Marehemu aliacha nyumba moja iliyoko Mtaa wa Ntinginya, wilayani Nzega yenye namba NTC/NMSH/NTI/81.

Katika uamuzi wake wa awali, mahakama iliamuru msimamizi wa mirathi awasilishe mahakamani orodha ya mali za marehemu, alipe madeni aliyoacha marehemu kama yapo na apewe mirathi.

Wanafamilia katika mirathi hiyo ni wajukuu Araf Seager, Azaz Seager, Haji Seager, Asha Seager, Gullam Seager, Fatuma Seager, Kasu Seager na Karim Samji ambaye ni mtoto.



Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM wilaya ya Kinondoni, Wakili Mharami Chuma (katikati), akikabidhi sehemu ya msaada wa vitu mbalimbali ikiwemo vyakula kwa Mkuu wa Kituo cha Watoto yatima cha Mother of Mercy Madale, Sista Christina Christopher, vilivyotolewa na Jumuiya ya Wazazi Kata ya Wazo, kuadhimisha miaka 47 ya CCM, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mwenyekiti wa Wazazi wa Kata hiyo, Jesca Mrope (wa tatu kushoto), Mwenezi wa CCM Kata ya Wazo, Hawa Mafumbi, Mwenyekiti wa UWT wa Kata, Doris Mrimi (kushoto), Katibu wa EMMA wa wilaya hiyo, Mhandisi Johnson Kashasha (kulia) na Katibu wa Wazazi wa kata hiyo, Rehema Salama. **PICHA: JOHN BADI**

# Kamati ya Maadili ya kitabibu yaanzishwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TANZANIA imekuwa nchi ya kwanza Ukanda wa Afrika Mashariki kuanzisha Kamati ya Maadili ya Kitabibu kwa ajili ya kushughulikia vikwazo vya maadili wanavyokutana navyo matabibu wakati wa kutoa huduma kwa wagonjwa.

Programu hiyo inasimamiwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Oslo cha Norway kupitia programu iitwayo ETHIMED.

Akizindua programu hiyo jana katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH), Mratibu Lucas Kitula alisema kamati hiyo inayojumuisha watu 12 wakiwamo madaktari, wafamasia, wanasheria na viongozi wa dini, inalenga kushughulikia vikwazo mtanziko wa kimaadili (ethical dilemma) wanavyokutana navyo watoahuduma za afya wakati wa kutoa huduma kwa wagonjwa.

"Mwaka jana tulianza kutoa mafunzo ya maadili ya kitabibu kwa watoa huduma za afya na wakufunzi hapa na leo (jana) tunaanza mafunzo ya siku nne kwa ajili ya kuwajengea uwezo wanakamati.

"Programu hii ni ya miaka mitano na tumeanza na hospitali hii ili tuweze kupima mafanikio, baadaye tunatarajia kuanzisha kamati za maadili kwenye hospitali zote nchini.

"Baada ya mafunzo kamati hii itakutana na watoahuduma za afya kuwapa elimu ili wanapokutana na mtanziko wa kimaadili wakati wa kutoa huduma wawasilishe kesi hizo kwenye kamati ili kupata ufumbuzi wa pamoja utakaomwacha mtoahuduma na mgonjwa wote wakiwa salama," alisema Kitula.

Mkuu wa Idara za Falsafa na Taaluma za Dini UDSM ambao wanasimamia programu hiyo, Dk. Michael Lyakurwa, alisema kamati hiyo haina uhusiano na ile ya kinidhamu, bali yenyewe itajikita kufanya utafiti, kutafakari na kujadili mambo kabla hayajatokea ili kufanya uamuzi sahihi.

Alisema wakati mwingine watoahuduma za afya wanaweza kufanya uamuzi ambao utasababisha mgonjwa kuishtaki hospitali, hivyo kamati hizo zitakuwa na kazi ya kusaidia watoahuduma za afya wanapokutana na mtanziko kupeleka kesi zao kwenye kamati hiyo ili kujadili njia ya kufikia uamuzi sahihi.

Mkufunzi wa Maadili ya Kitabibu kutoka Chuo cha Oslo cha Norway, Dk. Berit Larsen, alisema waliamua kushirikiana na Tanzania kuendesha programu hiyo ili kushirikisha uzoefu wao wa zaidi ya miaka 25 ambao wamekuwa nao kwenye hospitali zao zote ambazo zina Kamati ya Maadili ya Kitabibu.

Aliongeza kuwa wanaamini kuwapo kamati hiyo kutaboresha utoaji huduma za afya nchini kwa kuwa zipo changamoto za kitabibu zinatokea ambazo hazihitaji kamati za kinidhamu zenye jukumu la kuwajibisha, bali zinahitaji kutafuta suluhisho pasi na kuadhibu.

Akizindua mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji alisema kwa muda mrefu watoahuduma za afya walishindwa kukabiliana na mtanziko wa kimaadili wakati wa kutoa huduma kwa wagonjwa kwa sababu hawakuwa na mahali pa kufikisha matatizo yao, hivyo kamati hiyo inakwenda kuleta suluhu.

Dk. Mbwanji alisema kamati hiyo itasaidia kupunguza malalamiko na kesi ambazo zimekuwapo baina na wagonjwa na watoahuduma kwa kuwa taratibu za kimaadili zitakuwa zimefuatwa.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk, Rehema Marando alisema italeta suluhisho la mtanziko wa kimaadili kwa watoahuduma za afya kwa kuwa inatoa nafasi ya majadiliano ya pamoja ambayo yatasaidia kufikia uamuzi utakaoboresha utoaji huduma kwa wagonjwa.

## Sheria mpya kudhibiti ubadhirifu Ushirika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI iko mbioni kufanya mabadiliko ya Sheria ya Vyama vya Ushirika ili kukomesha vitendo vya ubadhirifu vinavyofanywa na viongozi wasio waadilifu.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alibainisha hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Mbozi (CCM), George Mwenisongole.

Mbunge huyo alihoji sababu za watuhumiwa wanaokamatwa kwa makosa yanayohusiana na mali za ushirika kushtakiwa kwa kesi ya madai badala ya kosa la uhujumu uchumi.

Alitaka viongozi wote wa vyama hivyo waliowaibia wakulima wafikishwe mahakamani kwa kosa la uhujumu uchumi na si madai.

Waziri Bashe alisema watuhumiwa hao wanashtakiwa kwa kesi ya madai kwa kuwa mamlaka na uwezo wa wizara ni kufanya uchunguzi na wanapomaliza hukabidhi kwa vyombo vya dola.

"Vyombo vinaangalia kesi yenyewe na kupeleka mahakamani kwa mujimu wa sheria. Ni kweli mara nyingi wanaofanya ubadhirifu kwenye vyama vya ushirika kesi zao zinaishia kuwa za madai na kulipa fedha.

"Katika mchakato wa Sheria ya Vyama vya Ushirika tutakayoleta bungeni, tutakuwa na kipengele kitakachoeleza namna gani ubadhirifu utakaofanyika watuhumiwa watapewa adhabu kali na wasitumie vibaya nafasi zao," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Kisesa (CCM), Luhaga Mpina alihoji chimbuko la ubadhirifu kwenye vyama hivyo.

Waziri Bashe, akijibu swali hilo, alisema kwa vyama vingi vya ushirika vimeanza kupata hati safi kwenye ukaguzi na ubadhirifu umeendelea kupungua.

"Ni kweli ubadhirifu bado upo na sababu kubwa ni ukosefu wa uadilifu kwa wanaopata nafasi kwenye uongozi na sababu nyingine ni mfumo wa kuwapata viongozi wa vyama vya ushirika. Mabadiliko ya sheria yatakayokuja yataweka mfumo wa kuchuja viongozi wa vyama wasio waadilifu," alisema.

Awali katika swali la msingi, Mbunge Mwanisongole alihoji lini serikali itamaliza uchunguzi kwa vyama vya AMCOS – Mbozi ambavyo havikupatiwa uchunguzi wa awali.

Bashe akijibu swali hilo, alisema kwa mwaka 2023/24 AMCOS nane kati ya 20 wilayani Mbozi, mkoani Songwe zimebainika kuwa na ubadhirifu na waliobainika wamechukuliwa hatua na kuwafikisha kwenye vyombo vya dola.

Alisema vyama hivyo vilipofanyiwa uchunguzi na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Sh. milioni 170.2 zimerejeshwa na jitihada zinaendelea ili kurejesha kiasi kilichobaki cha Sh. milioni 124.6.

Alibainisha kuwa hadi sasa, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) limekagua AMCOS 157 kati ya 217, na kati yake, AMCOS 60 ziko kwenye mpango wa kukaguliwa na kukamilika ifikapo Machi 2024.

"Hatua hii ni sehemu ya jitihada za serikali kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika ushirika na kuwachukulia hatua viongozi watakaobainika kuhusika na ubadhirifu wa mali na fedha za vyama husika," alisema.

TANGAZO

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

## TAARIFA KWA UMMA

## BEI MPYA ZA STEMPU ZA KODI ZA KIELEKTRONIKI (ETS)

**Dar es Salaam, 5 Februari, 2024:**
Kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (2) ya Kanuni za stempu za kodi za kielektroniki za mwaka 2018, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) anapenda kuwatangazia bei mpya za stempu hizo kufuatia majadiliano yenye mafanikio makubwa kati ya Mamlaka ya Mapatao Tanzania (TRA), Umoja wa wenye viwanda Nchini Tanzania (CTI) na mkandarasi SICPA SA. Watengenezaji, Wazalishaji na Waagizaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa na ambazo zimeorodheshwa katika jedwali la kwanza la kanuni za kodi za kielektroniki za mwaka 2018 watanunua stempu hizo kutoka kwa muuzaji aliyeingia mkataba na TRA kwa bei zilizoorodheshwa hapo chini.


Bei hizi mpya zimeanza kutumika kuanzia tarehe **24 Januari, 2024**. Kwa maelezo zaidi tembelea ofisi ya TRA iliyopo karibu nawe au tembelea tovuti ya TRA **www.tra.go.tz** au piga simu bure kwenda namba **0800-780078** au **0800-750075** au **0800-110016,** WhatsApp **0744-233 333** au Barua pepe **services@tra.go.tz.**

| Na. | Aina ya Bidhaa | Chanzo | Bei ya zamani kwa '1000' | Bei Mpya kwa '1000' |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Pombe kali, na pombe kali za mvuke | zote | 42,214.37 | 33,392.00 |
| 2 | Mvinyo wa zabibu n.k | zote | 42,214.37 | 33,392.00 |
| | Mvinyo wa matunda kama vile ndizi na nyanya n.k | Wenye matunda ya ndani kwa asilimia 75% au zaidi | 17,435.37 | 11,482.00 |
| 3 | Sigara au bidhaa mbadala wa tumbaku | zote | 42,214.37 | 29,854.00 |
| | Bidhaa nyingine za tumbaku n.k | zote | 42,214.37 | 29,854.00 |
| 4 | Bia n.k | Zinazozalishwa nchini | 18,312.91 | 14,857.00 |
| | Bia iliyotengenezwa kwa kimea n.k | Zinazoingizwa kutoka nje | 23,093.20 | 17,795.00 |
| 5 | Juisi za matunda na mbogamboga | Zinazozalishwa nchini (kwa matunda ya ndani) | 8,082.62 | 6,889.00 |
| | Juisi ya matunda ikiwemo ya zabibu, juisi ya mbogamboga zisizowekwa chachu. | Zinazoingizwa kutoka nje | 15,264.51 | 10,068.00 |
| 6 | Maji ya chupa | zote | 8,082.62 | 6,889.00 |
| 7 | Vinywaji laini au maji yaliyoongezwa ladha na vinywaji vingine visivyo na kilevi bila kujumuisha juisi za matunda. | Zilizo chini ya Tariff namba. 2202.10.00 | 8,082.62 | 6,889.00 |
| | Vinywaji laini au maji yaliyoongezwa ladha na vinywaji vingine visivyo na kilevi bila kujumuisha juisi za matunda. | Vinywaji vingine chini ya tariff namba 2202.91.00 na 2202.99.00 | 15,264.81 | 10,068.00 |
| 8 | Bidhaa za filamu na muziki (Yaani CD/VCDs/dvd/kanda zilizorekodiwa | zote | 16,165.24 | 16,165.24 |

Imetolewa na;

A.J.Kidata

**Kamishna Mkuu**





# Mikataba saba yasainiwa kumaliza kero ya maji katika vijiji 17

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme ameshuhudia utiaji saini wa mikataba saba ya utekelezaji miradi ya maji yenye thamani ya Sh.bilioni 6.4 itakayotekelezwa katika wilaya za Kahama, Kishapu na Shinyanga.

Miradi hiyo inayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 inatarajiwa kumaliza tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika vijiji 17 katika wilaya hizo.

Akizungumza baada ya utiaji saini wa mikataba hiyo, Christina aliwataka makandarasi wazawa ambao wamepewa miradi hiyo, kuitekeleza kwa viwango stahiki ili iendane na thamani ya fedha pamoja na kuhudumia wananchi kwa muda mrefu.

Alisema serikali imewaamini makandarasi wazawa na kuwapatia mikataba hiyo na kuwataka waikamilishe kwa wakati, ili wananchi waanze kupata huduma ya majisafi na salama na kuondokana na matumizi ya maji ya kwenye mabwawa pamoja na mito.

Alisema kwa sasa hali ya upatikanaji maji katika maeneo ya vijijini mkoani hapa ni asilimia 66 na kwamba hadi kufikia mwaka 2025 upatikanaji wa maji vijijini utakuwa asilimia 85.

Vilevile, aliwataka wananchi kuitunza miundombinu ya miradi ya maji pamoja na kutumia maji safi na salama na yaliyotibiwa na mamlaka husika na kuacha matumi ya kwenye mito na mabwawa yanayohatarisha afya zao na kusababisha mlipuko wa magonjwa.

Meneja Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Shinyanga, Juliety Payovela, alisema kati ya mikataba hiyo saba, miradi sita itahusika kwenye ujenzi wa miradi ya maji na mradi mmoja ni wa ununuzi wa bomba pamoja na viungio.

Alisema miradi yote inatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka mmoja kutoka sasa.

Naye mmoja wa makandarasi wazawa, Stephen Owawa kutoka kampuni ya Geo Statia Classic Works Ltd, akizungumza kwa niaba ya wenzake waliosaini mikataba hiyo, alisema hawataiangusha serikali bali wataitekeleza kwa wakati na ubora unaohitajika.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Mohamed Mfaki, akizungumza na wakuu wa shule za sekondari za wilaya katika ofisi ya mkuu wa wilaya hiyo, Lusanga juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wasichana walioachishwa masomo wawezeshwa ujuzi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WASICHANA 263 walioachishwa masomo katika mikoa ya Shinyanga na Mara kwa sababu mbalimbali wamepewa mafunzo ya ujuzi katika kada tofauti pamoja na kupewa vifaa kwa ajili ya kuwainua kiuchumi.

Vifaa hivyo vyenye thamani ya Sh.milioni 80 vimetolewa kupitia mradi wa 'chaguo langu haki yangu' chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo Afrika WiLDAF kwa kushirikiana na UN-FPA kwa wasichana hao.

Vilevile wamewezeshwa kuendelezwa kimasomo katika katika vyuo vya ufundi katika fani za ushonaji, ufundi umeme, ususi, ufundi magari, ufundi bomba, uendeshaji wa mitambo ya barabara pamoja na uchomeleaji.

Mratibu wa mradi huo, Joyce Kessy, alitaja vifaa vilivyotolewa kuwa ni pamoja na vyerehani 53, mashine moja ya kudarizi na mkasi wake, vikausha nywele 17, beseni za kusafisha nywele 17.

Vingine ni seti za vitana mbili, rolazi za mifuniko seti 17, rolazi za miba seti 17 pamoja na vifaa vingine muhimu vya ususi, huku akiwataka kuvitumia vema ili viwanufaishe na kuwainua kiuchumi.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba akizungumza wakati wa kukabidhi vifaa hivyo jana alisema wasichana wenye ujuzi mbalimbali watapatiwa kazi katika ujenzi wa barabara za zinazofadhiriwa na Benki ya Dunia (WB) wilayani wilayani hapa.

Mabinti hao ni wale wenye ujuzi wa ufundi umeme (3), ufundi magari(1), ufundi bomba(3), uendeshaji wa mitambo ya barabara(1) pamoja na mchomeleaji (1) wanaotoka katika mazingira magumu.

Alisema mabinti hao watatakiwa kuandika barua za kuomba kazi hiyo, huku akiahidi kuwasimamia na kuhakikisha wanapata fursa hizo zinazoendana na ujuzi walio nao.

Pia aliwataka wale wenye ujuzi wa uchonaji, udarizi, mapambo, sekretari na mapishi, kutengeneza vikundi kwenye kata zao ili wawe na sifa ya kupata mikopo isiyokuwa na riba inayotolewa na halmashauri ili waweze kupata fedha za mitaji na kulipa pango la ofisini.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita alilipongeza shirika hilo kwa kuwapatia ujuzi mabinti waliopo katika mazingira magumu utakaosaidia kutojiingiza kwenye vishawishi vitavyosababisha kupata maambukizi ya VVU na kuahidi kazi zote zinazokuwa zinapatikana katika sekta ya afya na elimu watapewa kipaumbele.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Kahama, Swaiba Chemchem aliahidi kushirikiana na maaofisa maendeleo ya jamii walipo kila kata katika kuhakikisha mabinti hao wanakuwa kwenye vikundi vya ujasiriamali ili wawe na sifa ya kupata mikopo ya asilimia 10.

# Mahakama yafuta mashtaka ya mchungaji dhidi ya DC

**Na Zatifa Ramadhani,** SAUT

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Mwanza imefuta maombi madogo ya shauri namba 68/2013 yaliyopelekwa dhidi ya Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi na mleta maombi mchungaji, Bensoni Kitonka wa Kanisa la Assemblies of God Gospel Church International (AGGCI).

Mahakama hiyo imefuta maombi hayo kutokana na hoja zilizowasilishwa kutokuwa sahihi.

Hatua hiyo imefikiwa juzi na Jaji wa Mahakama Kuu, Wilbert Chuma na kutaja sababu kuwa hoja zilizotolewa na mjibu maombi kwamba kilichotakiwa kushtakiwa ni cheo/ofisi wala siyo mtu kama ilivyowasilisha shtaka dhidi yake.

Jaji Chuma alisema Mahakama iliona ni kosa kwani hoja ikishaibuliwa hairuhusiwi tena kubadilisha upungufu kwa wakati huo, hivyo kuamua kuiondoa moja kwa moja mahakamani hapo.

Aidha alisema maombi ya kubadilishwa shauri hilo yaliyotolewa na upande wa mleta maombi kufuatia kiapo kinzani cha mjibu maombi kuonesha maombi hayalandani na hoja tajwa, hivyo kutoa fursa ya maombi hayo kuletwa upya mahakamani hapo kama rufani.

Jaji Chuma alisisitiza kuwa kazi ya kiapo ni kulandana na zile hoja zilizotajwa katika madai, hivyo kama hoja ya kwanza ingekuwa sawa basi hakukuwa na sababu ya kujadili hoja ya pili na Mahakama haiwezi kuendelea kuzungumza maombi kwa sababu majina yalikosewa.

Akizungumza nje ya Mahakama hiyo, wakili wa mleta maombi, Gibson Ishemgoma alieleza kupokea uamuzi wa Mahakama hiyo na kusema kuwa bado wanao uwezo wa kupeleka shauri jipya kwa kusahihisha makosa hayo ya kukishitaki cheo na sio jina la Mkuu wa Wilaya.

"Mahakama imetoa maamuzi na kutupa nafasi ya kukata rufaa na kusahihisha makosa ya kiuandishi lakini mteja wangu ameonesha kutokuwa na nia ya kuendelea na kesi hiyo". alisema wakili Ishengoma

Mchungaji wa kanisa hilo, Benson Kitonka alisema kwa imani yao wameamua kuwaachia waumini wengine kwani kilichowatenganisha wao ni majina tuu lakini wote ni waumini wa imani moja na muasisi wao alikuwa ni Moses Kulola.

Hivyo aliomba kurudishiwa vitu vyao ili wakatafute sehemu nyingine na waweze kuanzisha shughuli za ibada kama ilivyo kawaida.







siasa
JUMATANO FEBRUARI 7, 2024
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

MRITHI WA MREMA TLP...

# Wazidi kuvurugana,wanachama sasa kumchagua M/kiti kibabe

- Viongozi walaumiwa wawajibu wanaowatishia, hawatambuliki

**Na Sabato Kasika**



Mwenyekiti wa Vijana TLP, Aivan Maganza (wa pili kushoto) na wajumbe wenzake wakizungumzia uchaguzi huo. Kulia ni mjumbe kutoka Kusini Pemba, Mohamed Seif Mohamed, mwingine ni Mariam Omary Khamisi wa Kaskazini Pemba na kushoto ni kutoka mkoa wa Dodoma, Damary Richard. **PICHA: SABATO KASIKA**

MZIMU wa Augustine Mrema, bado unakiandama Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), kikiendelea kukwama kupata mwenyekiti baada ya kifo chake, sasa kikielekea kuparanganyika.

TLP iko ndani ya sintofahamu kutokana na wajumbe wa Kamati Maalum ya Mkutano Mkuu wa Uchaguzi kufanya maamuzi yanayotishia kukisambaratisha chama chao wakidai ni kutokana na kushindwa kuitisha uchaguzi mkuu na kuchagua mwenyekiti wa taifa.

Kamati hiyo mwishoni mwa mwezi uliopita iliupa uongozi wa chama hicho unaoongozwa na Kaimu Mwenyekiti Taifa Hamad Mukadam, siku saba kuitisha haraka uchaguzi wa mwenyekiti vinginevyo wajumbe hao wataitisha wenyewe uchaguzi huo.

Tangu kifo cha mwenyekiti wa taifa Mrema, Agosti 21, 2022 chama hakijafanya uchaguzi zaidi kuendelea kukaimisha uongozi.

Mara baada ya kifo chake, ilipofika Septemba 2022, sekretarieti ya chama hicho ilimchagua Hamad Mkadamu, kukaimu nafasi hiyo kusubiri uchaguzi kwa muibu wa katiba.

Hata hivyo, uchaguzi umekuwa ikiharishwa mara kwa mara, hatua ambayo imesababisha wajumbe kuja juu na sasa uvumilivu umewashinda na kuamua kuweka wazi kwamba wanataka uchaguzi.

**MWISHO LEO**

Mwenyekiti wa Vijana wa TLP, Ivan Maganza ambaye alikuwa mmoja wa waliogombea nafasi ya mwenyekiti taifa, akizungumza na gazeti na baadhi ya wajumbe wiki iliyopita, anasema siku saba zinaisha leo Februari 7 na kwamba wakiendelea kuwa kimya, wataitisha uchaguzi.

"Nilizunguka nchi nzima kukusanya saini za wajumbe wa mkutano mkuu wa uchaguzi, karibu wote wanataka uchaguzi ufanyike," anasema na kuhoji wanakwama wapi?

Anafafanua kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu walikuwa 80, lakini kwa sasa wamebaki 70 baada ya wengine kufariki dunia na baadhi yao kuhama chama, na kwamba hao 70 wamesaini kuonyesha wanahitaji uchaguzi ufanyike.

Maganza anasema, tangu mwanzoni mwa mwaka jana hadi Januari mwaka huu, uchaguzi umekuwa ukiahirishwa bila sababu za msingi, na kwamba kitendo hicho kimewakera wajumbe.

"Uchaguzi ulipangwa kufanyika Januari 8 mwaka jana, ukaahirishwa hadi Machi 6 mwaka huo, haukufanyika, ukapangwa kufanyika Mei mosi 2023 lakini pia haukufanyika," anasema Maganza.

Anasema, baada ya hapo ukapangwa kufanyika Desemba 28 mwaka jana, lakini ukakwama, baadaye ukasogezwa hadi mwezi uliopita (Januari 28), lakini pia zikawa danadana.

"Chanzo cha yote haya ni katibu mkuu ambaye naye alikuwa anagombea nafasi ya mwenyekiti, alipobaini kuwa hakubailiki, akavuruga uchaguzi," anasema.

Anadai, kutokana na mazingira hayo, wajumbe wamechoka na sasa wametoa siku saba kwa uongozi, ambazo zimeisha leo Februari 7, na kwamba iwapo utashindwa kuitisha uchaguzi, wao wataitisha ili ufanyike kabla ya kumalizika mwezi huu.

Mgombea Maganza anasema, wanataka wajiandae kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa na kwamba ni muhimu chama kiwe na uongozi mpya.

Anasema, siku hizo saba zilianza Januari 29, na kwamba hawatarudi nyuma katika hilo kwa kuwa wameshapeleka barua za kutaka uchaguzi, katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

"Ibara ya 24 ya Katiba ya TLP, inaeleza kuwa nafasi ikiwa wazi ijazwe mara moja, lakini tangu tulipopata kaimu mwenyekiti, hadi leo uchaguzi unapigwa chenga," anasema.

Aidha, anataja, ibara 21.3 (a),inaelekeza kuwa wanachama na viongozi wote wanajitolea kufanya uchaguzi, hakuna malipo maalum kwenye vikao, na kwamba wanatimiza majukumu yao kwa kujitolea.

"Hivyo, katibu na kaimu mwenyekiti wasikwepe kuitisha mkutano wa kigezo cha gharama kwani wajumbe wenyewe wanajigharimia, lakini pia ibara ya 18.5 (k), kazi ya halmashauri kuu ni kuandaa mkutano mkuu. Ndiyo inayotumika kuandaa kamati maalum kutoka halmashauri kuu ili kusimamia na kuandaa mkutano mkuu kuziba nafasi ya mwenyekiti wa taifa," anasema.

**ATHARI**

Mwenyekiti Kamati Maalum ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu ambaye pia ni Katibu wa TLP mkoa wa Dodoma, Damary Richard, anasema, kutofanyika kwa uchaguzi kunasababisha chama kupoteza hadhi.

Damary anaelekeza lawama kwa kaimu mwenyekiti wa chama hicho, Hamad Mkadam na Katibu Mkuu Richard Lyimo,

**INAENDELEA UK. 14**

ACT INAPOIPASHA SERIKALI

# Sukari, usafiri ni misumari inayowatesa zaidi maskini



Waziri Kivuli wa Uchukuzi ACT Wazalendo, Kiza Mayeye, akizungumzia machungu ya usafiri kutokana na kupandisha nauli. **PICHA: HALFANI CHUSI**

**Na Halfani Chusi**

KUPANDA kwa bei ya sukari na nauli, kunakiibua Chama cha ACT Wazalendo, kuishauri serikali kutatua adha hiyo ambayo inawagandamiza wananchi wengi maskini.

Kama ilivyo nadharia ya wahenga, mtembea bure si sawa na mkaa bure, ndivyo kinavyoamini chama hicho kwamba dai lao dhidi ya serikali litarejea na majibu chanya.

Ni Halima Nabalang'anya, Waziri Kivuli wa Viwanda na Biashara wa ACT-Wazalendo, anayehadharisha kuwa kupanda kwa bei ya sukari ni mzigo mzito kwa wananchi maskini.

Akizungumza na wanahabari Dar es Salaam, hivi karibuni, anasema tatizo kubwa linalowaelemea Watanzania wenye kipato kidogo na kupanda bei mara dufu kunawaumiza zaidi.

Anakumbushia kuwa hali hiyo ilianza mwishoni mwa mwaka jana na sasa imezidi kuwa mbaya akisema bei ya bidhaa hiyo kwa rejareja katika mikoa mbalimbali ni kati ya Sh. 4,000 hadi 6,000 kutoka bei ya Sh. 2,500 au 2,800 mwaka, Juni mwaka jana.

"ACT tunaona kauli, hatua na miongozo ya serikali, havisaidii kutoa nafuu ya bei ya sukari tofauti na ahadi na hadaa inazozitoa. Kushindwa kuzalisha mahitaji yetu ya ndani ni sababu kubwa sana inayofanya tushindwe kudhibiti upandaji wa bei za bidhaa mara kwa mara.

"Uwezo wetu wa kuzalisha bidhaa kwa matumizi yetu ya ndani ni mdogo mno, mahitaji ya sukari kwa mwaka ni tani 585,000 wakati uwezo wa kuzalisha ni tani 370, 000. Zinapelekea tani 215,000 tunazoagiza kutoka nje," anasema Halima.

Anaikosoa serikali kuwa ina wepesi wa kutoa vibali vya kuagiza sukari kuliko kutoa vya kuzalisha na kuhakikisha kunakuwa na viwanda vya kutosha vinavyotengeneza sukari.

"Tatizo la sukari kibiashara ni kama lango la ulanguzi na kujilimbikizia mali kwa baadhi ya wafanyabiashara wanaoagiza. Hivyo, uzalishaji wa sukari ndani kwao unawaondolea faida ya ziada (surplus profit).

Ndiyo maana zipo hisia au ushahidi wa kukamatwa kwa zaidi ya tani 40 mkoani Mtwara zilizofichwa ikiwa ni mbinu ya kutengeneza uhaba ili kupandisha bei," anasema Waziri Kivuli.

Anabainisha kwamba tatizo la sukari limekuwa kama wimbo wa taifa na kila mwaka linapotokea tatizo hilo inakuja na kauli za hadaa kuwa itamaliza tatizo hilo, lakini tangu uhuru mpaka sasa hakuna jipya.

Anasema chama chao kina wasiwasi kauli na ahadi hazisaidii kutatua tatizo liliopo, kinashangaa kuona serikali kupitia bodi ya sukari imetoa bei elekezi ya kati ya Shilingi 2,600 na 3,200.

Anaongeza kuwa haiakisi uhalisia wa gharama za manunuzi wa bidhaa hiyo ambayo bado ni ghali na haiwezi kuuzwa kwa bei hiyo, huu ni mwendelezo wa serikali kuwachezesha na kuwahadaa wananchi.

Anakumbushia kuwa Waislamu wanakaribia kwenda kwenye Mfungo wa Ramadhani wakati Wakristo wanakaribia kuanza Kwaresma Jumatano ijayo hivyo ni lazima serikali iondoe adha hiyo ili wananchi wasiendelee kupata shida.

"Tunaitaka iweke nguvu kubwa kuhakikikisha upatikanaji wa kutosha wa sukari serikali kupitia vyombo vyake ifuatilie mwenendo wa uingizaji, uuzaji na usambazaji ili bei ishuke na wananchi waipate kwa wakati na kwa bei nzuri." Anasema.

Anaongeza: "Tunaitaka kuongeza kasi ya uwekezaji na uzalishaji katika viwanda kwa kuweka mazingira bora ya kisera na kisheria na kuchochea matumizi ya teknolojia za kisasa hasa kwenye kiwanda cha Mkulazi mkoani Iringa.

Kinazalisha tani 46 tu za sukari kiwe na uwezo mkubwa wa kufikia tani nyingi zaidi kukabiliana na changamoto mbalimbali katika soko la bidhaa hiyo."

Anashauri kuvifuatilia viwanda vikubwa saba vinavyozalisha sukari na kutia mkazo uzalishaji wa ndani wa kwa kuzingatia vipindi mbalimbali vya hali ya hewa, kutumia teknolojia ya kisasa, mvua iwe fursa na neema kwa wakulima na kilimo wala si kikwazo na hilo litawezekana kutumia teknolojia, sera na mifumo rafiki.

## KUPANDA NAULI

Kuhusu kupanda kwa nauli Waziri Kivuli wa Uchukuzi, Viwanda na Biashara, Kiza Mayeye, anasema tangu Desemba mwaka jana kumekuwapo na ongezeko la nauli za mabasi ya abiria kote nchini.

Hatua hiyo inakuja kufuatia tamko la serikali linalotolewa na Wakala wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) kutangaza bei mpya, lakini zinazowaumiza wasafiri na wafanyabiashara.

Kiza anasema ongezeko hilo ni la nauli za daladala zimefikia wastani wa kati ya Sh. 270 hadi 400 kwenye Sh.1,000.Kwa lugha nyingine ongezeko kwa nauli za daladala limepanda kwa asilimia 27 hadi 40 katika maeneo mbalimbali nchini.

Anatoa mfano wa Dar es Salaam kuwa nauli ya mwendokasi zimepanda kutoka Sh 650 hadi 750 na Kariakoo- Mbezi 1,050 hadi 1,200. Pamoja na uhaba mkubwa magari na kusababisha msongamano na usumbufu kwa abiria.

"Kwa upande wa nauli za mabasi ipo shida kubwa sana ongezeko limekuwa asilimia 18 hadi 36 kwa baadhi ya mikoa. Nauli za mabasi ya masafa marefu ni kubwa ongezeko la nauli hii linakuwa ni kubwa sana," anasema Kiza.

Anasema katika uchambuzi wamegundua hoja wanazozitoa LATRA zinalalamikiwa kuwa zinalenga kujenga uhalali wa kuwakandamiza wananchi lakini zikiwatengenezea faida kubwa wafanyabiashara hasa wasafirishaji.

Kiza anazungumzia hoja ya kupanda bei ya mafuta, inayotumika mara kwa mara kama kichaka kupandisha bei na mara kwa mara wafanyabiashara wa mabasi hutumia, lakini inashangaza inatumika kwenye kupandisha pekee mafuta yanaposhuka nauli zinabaki zilivyo.

Anasema kwa sasa inashuhudiwa kushuka kwa mafuta katika soko la dunia, akisema haiwezi lakini hilo halionekani kwenye kushuka kwa nauli.

Hussein anazungumzia hoja ya gharama za uendeshaji kuongezeka ni za kutengenezwa kwa kuwa gharama halisi za uendeshaji zinahusisha mishahara ya wafanyakazi, matengenezo na vipuri, mishahara na stahiki za wafanyakazi ikiwamo madereva, wasaidizi, wakatisha tiketi hazijaongezeka.

"Madai ya kuongezeka bei za vipuri yanaweza kuwa si sahihi kwa vile kwa sasa vipuri katika soko vimepungua kutokana na idadi kubwa ya waagizaji walioko nchini." Anaongeza.

Anasema hata mishahara na huduma nyingine kwa wafanyakazi hazikuongezeka kama inavyodaiwa na kueleza kuwa mengi ni vingizio.

"Tozo na ushuru wa halmashauri, Kwanza sio kweli kiwango cha tozo kimesababisha kuongeza kwa kiasi hicho, ni aibu kwa halmashauri zinazoongozwa na CCM kukubali wananchi kuteseka kwa kuwaongezea mzigo wa tozo zaidi.

"Kitendo cha serikali kuridhia maamuzi ya Bodi ya LATRA inaonyesha haijajali kilio cha wananchi na kuamua kuwabebesha mzigo. Nauli hizi zimepanda sana, na haziakisi kipato cha Watanzania, zimeangalia maslahi ya wasafirishaji ambao ndiyo wafanyabiashara na watoa huduma na si hali za Watanzania walio wengi ambao ni maskini."

Kiza anasema chama hicho kinaitaka serikali kusitisha nauli mpya za mabasi ya masafa marefu na daladala, lakini kushusha gharama za uendeshaji kwa kurejesha ruzuku kwenye mafuta hasa dizeli na petroli.

Aidha, ACT inamtaka Waziri wa Uchukuzi kuimarisha Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Ardhini LATRA CCC, ili kuwa na nguvu katika uamuzi kwa kuongeza uwakilishi.

CCM +47

# Inataka wanawake viongozi wengi zaidi mashinani, bungeni na uongozi kitaifa

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI CCM inaposherehekea kutimizia miaka 47 ya kuanzishwa, inawataka wanawake kuchukua fomu kugombea uongozi wa vitongoji, vijiji na mitaa ili kufikia uwakilishi na uongozi wa uwiano wa 50/50, inapoelekea kufikia jubilii ya miaka hamsini.

Mwenyekiti wa UWT -Taifa, Mary Chatanda, anasema hayo, anapozungumza na Nipashe, wakati wa kumbukizi za kuzaliwa CCM Februari 5, 1977, ambazo zimefanyika juzi.

Anaeleza kuwa suala la kutegemea viti maalumu lisiwe tena kipaumbele badala yake vyama vihamasishe kinamama kujitokeza na kuchukua fomu za kuwania uongozi wa kuchaguliwa kwa ari, nguvu na mwamko zaidi.

Jumatatu Februari 5, CCM imetimiza miaka 47, baada ya kuviunganisha vyama vya AFRO-Shiraz ya Zanzibar na TANU ya Tanzania Bara.

Mwenyekiti wa UWT Taifa, anasema safari ya miaka 47 ya chama hicho ni jambo kubwa, akikumbusha kuwa siyo kila chama kilichoundwa Afrika kimefanikiwa kufikia hatua hiyo lakini kwa CCM imedumu na kufikia umri huo.

Anaongeza kuwa chama hicho kimeishi na kuongoza taifa, linaloshuhudia Watanzania wakitembea usiku na mchana katika maeneo mengi bila hofu kwa kuwa usalama na amani vipo, vikihimizwa na kusimamiwa na wananchi, chama na serikali.

Mary anakumbusha kuwa kuna mambo mengi ya kujivunia katika umri huo, akisema ni karibu kila kijiji kina shule na zahanati, umeme unawaka, kata zina vituo vya afya na sekondari, yote hayo yanang'arisha miaka 47 ya chama chake. kwa wananchi kuanzia ngazi za chini waliko Watanzania wengi.

Anagusia kuwa zipo nchi ambazo mambo ni magumu raia hawawezi kufurahia maisha na kujiletea maendeleo, lakini Tanzania kupitia uongozi wa CCM na serikali wananchi wanaishi kwa amani na kila mmoja anapambana kumudu maisha yake.

Anakiri kuwa serikali na chama vimefanya mambao mengi lakini bado juhudi zinahitajika akianza na suala la kufikia usawa wa kijinsia kwenye uongozi na uwakilishi kwa uwiano wa 50/50.

Anaeleza kuwa hilo ni suala muhimu, akivitaka vyama kulifanyia kazi kudumisha demokrasia na kufikia usawa kwa jinsi zote.

Mary anawatumia salamu kinamama akiwahimiza kujitokeza kuchukua fomu na kugombea uongozi wa vitongoji, vijiji na mitaa, unaofanyika mwaka huu.



Mary Chatanda Mwenyekiti wa UWT Taifa. **PICHA: CCM**

Anahimiza juhudi zifanyike ndani ya vyama kuwajengea wanawake uwezo, kujiamini na kuwapa mafunzo ya uongozi huku wakihamasishwa kushiriki na kugombea ili wawe sehemu ya mabadiliko ya kufikia uongozi wa 50/50.

"Tuwape mafunzo, tuwahimize kuchukua fomu kugombea uongozi wa vitongiji, vijiji na mitaa. Sisi kinamama ndiyo wapigakura wakuu tena wengi zaidi tuna jukumu la kufanikisha kuwepo uwiano wa nusu kwa nusu kiuwakilishi na kiuongozi."

**VIFO WAZAZI, WATOTO**

Mwenyekiti wa UWT, anapozungumza na Nipashe, anakemea suala la vifo vya wajawazito na watoto kutokana na kucheleweshewa huduma na uzembe wa wahudumu wasiojali.

"Hatunabudi kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan, amefanyakazi kubwa ya kuhakikisha nchi ina hospitali za kutosha. Ameboresha sekta ya afya. Karibu kila kijiji kina zahanati, kata zina vituo vya afya na kila wilaya ina hospitali ya rufani, lakini baadhi ya watumishi kwenye huduma hizo siyo waaminifu wala waadilifu."

> "Natoa wito jambo lolote linapotokea toeni taarifa polisi, kwenye vyombo vya dola. Sisi kinamama tuamke tukemee unapotokea ukatili tusinyamaze, tufuatilie tusikae kimya." anakumbusha.

Anazungumzia malalamiko yanayosababisha vifo vya wazazi, wajawazito na watoto, akisema baadhi ya watoa hudumu wanafanya kazi bila upendo na wengine hawana wito.

Mary anasema kutokana na kukosa ajira watu wanafanyakazi ambazo huenda hawana wito nazo ikiwamo ya uuguzi ya kuhudumia wazazi, wajawazito na wagonjwa na kusababisha mateso na hata vifo.

Mwenyekiti wa UWT, anasema nyakati hizi wasomi ni wengi wanaomba kazi ni wengi pia na kwamba muombaji akiajiriwa anafanya anavyopenda na kusababisha usumbufu kwa vile siyo wito wake.

Anatoa wito kwa madaktari, wataalamu mbalimbali wa afya, wauguzi na wakunga kufanya kazi ya kuhudumia wazazi, wajawazito na watoto kwa upendo na weledi bila kusababisha uchungu na mateso kwa wanawake.

Imekuwa kawaida kusikia taarifa za vifo vya wazazi na watoto zinazoripotiwa kwenye vyombo vya habari kutokana na kukosa huduma, uzembe na hata madai kuombwa rushwa.

Mwaka jana wauguzi katika Kituo cha Afya Tunduma walidaiwa kusababisha kifo cha mtoto mchanga kwa madai ya uzembe.

Aidha, tukio jingine ni mtoto mchanga kuvunjika mkono katika Hospitali ya Magunga iliyoko Korogwe mkoani Tanga, mkasa ukitokea mwezi uliopita.

Halikadhalika, Novemba mwaka jana mkoani Tanga katika kituo cha afya Kabuku wilayani Handani, mjamzito alifariki dunia kutokana na sababu kadhaa ikiwamo uzembe, kutojali kazi na pia kudaiwa fedha Sh.15,000 za upasuaji.

Mjamzito huyo na mwanawe walifariki baada ya daktari wa zamu, kupigiwa simu lakini hakufika kazini, aidha, mtaalamu wa nusu kaputi, alizima simu yote hayo yakasababisha wawili hao kufariki.

Pia, ripoti ya uchunguzi ya tukio hilo, ilieleza kuwa mwanamke huyo alikosa Sh.15,000 alizotakiwa kutoa ili kufanyiwa upasuaji kabla, vifo vyao viligusa mioyo ya wengi.

**UKATILI WATOTO**

Mwenyekiti wa UWT Taifa anazungumzia taarifa za ukatili kukithiri, ukitoka kwa mama na kuhamia kwa watoto na kutoa wito kwa kinamama na jamii kuripoti wasikae kimya uovu huo unapotokea.

"Natoa wito jambo lolote linapotokea toeni taarifa polisi, kwenye vyombo vya dola. Sisi kinamama tuamke tukemee unapotokea ukatili tusinyamaze, tufuatilie tusikae kimya." anakumbusha.

Anasema baadhi ya watuhumiwa wanajihusisha na ulawiti, ubakaji na kuwaingilia watoto kinyume cha wakiwamo wenye miaka mitatu na kinachoonekana hapo ni ushirikina na kutii maelekezo ya waganga.

"Wanawake wasikae kimya hata kama ni waume zao, matukio yakitokea, watoe taarifa za watuhumiwa, hata wakiachiwa tufuatilie tena tufunguke." Anasema.

Anasisitiza kuwa hata mambo yakitokea ndani ya nyumba wasiwafumbie macho waume, ndugu au yeyote mwana familia.

Anawataka Watanzania na kinamama kumuunga mkono Rais Samia na kukubali kazi zake kwa kuwa amethibitisha kuwa wanawake wanaweza.

Anakumbusha kuwa hapo awali watu walisema itakuwa rais mwanamama aongoze taifa? Samia anaongoza na amethibitisha kuwa ana uwezo na juhudi akiwataka Watanzania kumuunga mkono.

# Houthi kundi linaloishangaza dunia latikisa jeshi la Marekani, Uingereza

## • Lavuruga vituo, meli zake Ghuba ya Aden

**Na Moshi Lusonzo**

KUNDI la waasi la Wahouthi linalotawala Yemen, linaendelea kuzitetemesha nchi zenye nguvu kijeshi duniani kwa kuwa tishio katika biashara ya uckukuzi na usafirishaji inayotumia Ghuba ya Aden

Wahouthi wamejizatiti kurusha makombora kupiga meli zinazosafiri kwenye Bahari ya Shamu au Red Sea, ambayo ni mkono wa Bahari ya Hindi.

Bahari hiyo hupakana na Misri, Israel na Yordan upande wa kaskazini, lakini inapakana na Djibouti, Ethiopia, Somalia na Sudan kwenye pembe ya Afrika.

Bahari ya Shamu inaunganishwa na Bahari ya Mediteranian na mlango wa bahari wa Suez na pia kuna mlango mwingine bahari wa Bab El Mandab, unaoiunganisha na Bahari ya Arabia.

Ghuba ya Aden ni ukanda mkubwa wa usafirishaji wa shehena za meli zinazopitia kwenye mlango wa bahari wa Suez Canal kati ya Bahari ya Mediterranean na Bahari ya Arabia kwenda kwenye Bahari ya Hindi na kwa wastani meli 21,000 hutumia njia hiyo kila mwaka.

Marekani na Uingereza zimejinasibu kwamba zina uwezo wa kukomesha harakati za Wahouthi, lakini zimejikuta zikielekea kusalimu amri kutokana na kukabiliana na majibizano ya makombora na kupata hofu kama lengo lao linaweza kutimia.

Tangu Marekani na Uingereza kuanza mashambulizi kutumia ndege na meli za kijeshi kuharibu vituo kadhaa vya kijeshi vya Houthi, hakuna dalili ya kupungua kurusha makombora kuelekea meli zinazopita kwenye Bahari ya Shamu.

Wahouthi wanaendelea kuwashangaza wanajeshi wa mataifa hayo yenye nguvu, ambao hawajui ni namna gani wanaweza kuhimili vipigo vikali wanavyopata.

Aidha, wanagambo hao wanarusha makombora kwenye meli yoyote ya kimataifa inayomilikiwa na mataifa ya Marekani, Uingereza na Israel ikiwa ni kujibu mashambulizi ya Israel dhidi ya Wapalestina yanayoendelea huko Mashariki ya Kati.



Kiongozi wa Wahouthi, Abdul-Malik Badruldeen al-Houthi. **PICHA: MTANDAO**

Kulenga meli hizo kumeleta athari kubwa kwa biashara ya kimataifa na kuzilazimisha meli kuzunguka maelfu ya maili kukwepa kupitia Bahari ya Shamu.

Wachambuzi wanaeleza kuwa wanamgambo wa Kihouthi hawatishiki na mashambulizi ya mara kwa mara ya anga yanayoongozwa na Marekani kwenye vituo vyao vya makombora na wameapa kulipiza kisasi dhidi ya rasilimali za Marekani, Uingereza na Israel.

Wahouthi wanatokana na jamii ya watu wachache wenye asili ya eneo la milimani kaskazini-magharibi mwa Yemen na kwamba jina lao linatokana na mwanzilishi wa vuguvugu hilo, Hussein Al-Houthi.

Wapiganaji hao walishiriki katika vita kadhaa dhidi ya mtawala mwenye nguvu wa nchi ya Yemen, Ali Abdullah Saleh, mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Baada ya mtawala huyo kuondolewa madarakani kwa maandamano ya Arab Spring, waliteka mji mkuu, Sanaa, na kunyakua madaraka mwaka 2014.

Saleh aliingia vitani na Houthi, lakini kundi hilo lilifanikiwa kumkamata na kumuua na tangu Houthi wachukue mamlaka, Yemen ambalo ni taifa maskini zaidi la Kiarabu, limezidi kusambaratika kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyoendelea.

### KUSHAMBULIA MELI

Tangu kuanza harakati zake za kushambulia meli za kibiashara katikati ya Novemba 2023, Wahouthi wametumia kwa ustadi makombora na ndege zisizo na rubani kuzilenga meli zinazopita Bahari ya shamu.

Lengo la kuanzisha kwa mashambulizi hayo ni kulipiza kisasi kwa Israel kwa kuzizuia meli zenye uhusiano na Israel, Marekani na Uingereza zisikatishe kwenye bahari hiyo.

Hatua hiyo ni kuonyesha kuunga mkono kundi la Hamas ambalo linapigana na vikosi vya Israel katika Ukanda wa Gaza.

Wanamgambo wa Houthi ambao wengi wanafuata madhehebu ya Shia ni asilimia 15 ya raia wa Yemen, lakini wanaona wao ni watawala halali.

Balozi wa zamani wa Uingereza nchini Yemen, Edmund Fitton-Brown anasema kwa uzoefu wake na Wahouthi ni watu wenye hasira, uhasama na wakaidi.

“Ilikuwa changamoto kubwa. Walikuwa wakaidi, wenye uhasama, hasira, tabia ya kufoka, kuchelewa kufika na kususia vikao. Walisisitiza wapewe mapokezi ya heshima na kuwapa mirungi wakati wa mazungumzo ya amani anasema Brown.

Tangu waasi wa Houthi waanze mashambulizi dhidi ya meli, huku Marekani na Uingereza kujibu kwa kushambulia vituo vyao vya makombora, kumekuwa na maandamano makubwa yaliyoidhinishwa na serikali dhidi ya nchi hizo katika mji mkuu.

“Kwa kupinga kile ambacho wakazi wengi wa kaskazini mwa Yemen, wanakiona kama kundi la ukombozi na kuona serikali iliyotawala kama vikosi vya kigeni, na kulinganisha na Marekani, Uingereza na muungano unaoongozwa na Saudi Arabia,” anasema mtaalamu wa Mashariki ya Kati, Mohammed Al-Basha.

Al-Basha anaeleza kwamba kwa sasa Wahouthi wamepata umaarufu kutokana na njia wanazotumia kutawala na kwamba Yemen ya sasa inasalia kuwa taifa lililogawanyika, upinzani dhidi ya Houthi uko kaskazini-mashariki mwa Yemen, Maarib, Taiz na majimbo ya kusini.

Inaonekana dhahiri kuwa kuna uwezekano wa Houthi kuibuka washindi ikiwa kutakuwa na uchaguzi huru na wa haki ni dhahiri.

Kuhusu maandamano yaliyoandaliwa na Houthi, Fitton-Brown anasema utaratibu huo wanaufanya siku ya mapumziko ya kazi, na wanaweka wazi kwamba kila mtu anatakiwa kuhudhuria.

Wafanyakazi wao wengi waliajiriwa kwa sababu huko nyuma hawakuwa na ajira na walikuwa na hamu ya kupata kipato cha kila mwezi.

Katika maeneo ambayo yako nje ya udhibiti wao, kundi hilo linachukiwa kwa kuonekana watu wa vurugu.

Wahouthi wanamiliki ndege zisizo na rubani na silaha nyingine kali zinazoshambulia meli. Silaha nyingi zinatolewa na Iran na zingine zinaingizwa kimagendo kwenye boti ndogo au mipakani kwenye nchi kavu.

Akizungumzia mivutano hiyo itaishaje, Balozi Fitton-Brown anasema ikiwa usitishaji vita utafanyika Ukanda wa Gaza, wapiganaji hao wanaweza kuchukua fursa hiyo na kutangaza ushindi, wakidai wamefikia malengo yao na wao kuacha kushambulia meli.

Pia iwapo Iran itakuwa na wasiwasi kwamba vitendo vya Houthi vinaiweka nchi hiyo ya Kiislamu hatarini, ina ushawishi wa kutosha kuwafanya Wahouthi kubadili mwelekeo.

Anasema waasi wa Houthi bado wako imara licha ya kampeni za kijeshi na maeneo yao kurushiwa makombora na kuharibiwa.

Ni wazi kuwa wana makombora mengi, na kuna dalili wanatafuta njia ya kushambulia makombora ya kutoka ardhini hadi angani kwa nia ya kuangusha ndege za kivita za magharibi.

Hata hivyo, hali ya hatari itaendelea kuigubika Bahari ya Shamu na Ghuba ya Aden endapo mashambulizi haya ya kila upande yatazidi kuongezeka.

**BBC**

## WAZIDI KUVURUGANA,WANACHAMA SASA KUMCHAGUA M/KITI KIBABE

**INATOKA UK. 11**

kwamba wanaua chama kwa kupinga chenga kuitisha uchaguzi.

Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi kutoka Mkoa wa Kusini Pemba, Mohamed Seif Mohamed, anasema chama kimegeuzwa mali ya watu wawili walioamua kuvuruga uchaguzi na kukififisha nguvu zake.

“Kaimu mwenyekiti anakwepa kuitisha uchaguzi akidai hakuna fedha za kuandaa uchaguzi. Sisi tuko tayari kuugharimia, hivyo aache kutuhadaa na kufanya chama kikose nguvu mbele ya umma,” anasema Mohamed.

Mariam Omary Hamis, Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Uchaguzi kutoka Mkoa wa Kaskazini Pemba, anasema bila kuchukua maamuzi magumu chama hicho kitaendelea kudorora na hatimaye kufutika.

“Sisi wajumbe kutoka mikoa mbalimbali tumeamua kukusanya saini zetu ili kunusuru, hivyo tunawaomba viongozi wetu waitishe uchaguzi, na kama hawawezi, waondoke watuachie chama,” alisema Mariam.

### WATUHUMIWA WAJIBU.

Wakati wajumbe hao wakirusha tuhuma na kuwapa wiki moja ambayo imemalizika leo, Kaimu Mwenyekiti, Mkadam anasema hao si wajumbe halali, hivyo hawezi kuwasikiliza.

“Kama wangekuwa wajumbe halali, viongozi tungekutana nao na kupanga tarehe ya uchaguzi, hivyo suala la uchaguzi tutakutana wajumbe halali ili washauriane na kupanga tarehe,” anasema Mkadam.

Anafafanua kuwa yeye na katibu mkuu wa chama hawana taarifa za kukusanywa kwa saini za wajumbe hao, na kwamba hawawatambui, huku akiongeza kusema kuwa ni waasi tu ndani ya chama hicho.

Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, anasema, ofisi yake imepokea barua za malalamiko ya wajumbe hao kuhusu uamuzi wao wa kutaka uchaguzi ufanyike na kuahidi kuwa zitafanyiwa kazi.

“Wamefikisha barua zao katika ofisi yetu ya Dar es Salaam, na mimi sipo, hivyo ninaahidi kwamba nikirudi tutazifanyia kazi haraka iwezekanavyo,” anasema Nyahoza.



## Daktari ataja faida kuanzishwa wahudumu ngazi ya jamii

**Na Renatha Msungu** DODOMA

DAKTARI kutoka Shirika la Maria Stopes, James Mlali, amesema hatua ya serikali kuja na mfumo wa kuwatambua wahudumu ngazi ya jamii kutasaidia kuibua wagonjwa wenye changamoto mbalimbali hapa nchini.

Alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu umuhimu wa uzazi wa mpango pamoja na wahudumu ngazi ya jamii iliofanyika hivi karibuni.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo alisema kuna tatizo la wahudumu wa afya ikiwemo wengine kuzidiwa na idadi ya wagonjwa, hivyo hatua ya kuwatambua ikiwemo kuwawekea mfumo mzuri wa ufanyaji kazi kutapunguza msongamano wa wagonjwa.

"Tunashukuru sana serikali kutambua umuhimu wa wahudumu ngazi ya jamii kwa sababu itatengeneza idadi kwenye sekta ya afya, ikiwamo utoaji huduma kila kona," alisema Mlali.

Alisema kufanya hivyo pia kutasaidia watu wa pembezoni kufikiwa na huduma za kiafya pale wanapokuwa na changamoto za magonjwa mbalimbali.

Alisema awali wahudumu hao walikuwa wakifanya kazi kwa kushirikiana na sekta binafsi lakini sasa hatua ya kuanza kutambuliwa kutaongeza idadi ya utoaji huduma za afya.

Wiki iliyopita serikali ilizindua rasmi utambuzi wa wahudumu ngazi ya jamii utakaowezesha kusaidia kutoa huduma za afya katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema serikali imefanya hivyo ili wahudumu hao waweze kusaidia kuibua wagonjwa mapema kabla ya maradhi yao kuwa sugu na kushindwa kutibika.

Akitolea mfano magonjwa ya saratani, kisukari na figo, Waziri Ummy alisema wengi wao wanafika wakiwa katika hatua ya mwisho na matokeo yake kushindwa kumudu gharama za matibabu.

Kutokana na hilo alisema wameamua kuwatambua wahudumu ngazi ya jamii ili kusaidia kuwahimiza jamii kwenda hospitali, iliwemo kuwapatia huduma ya kwanza katika maeneo ambayo wanahusika.

Hata hivyo wahudumu hao hivi sasa wapo katika maeneo mbalimbali wengine wapo kwenye baadhi ya hospitali na kliniki wakitoa mwongozo kwa wajawazito.

Alisema wataendelea kushirikiana na wahudumu hao ili kuhakikisha wanasonga mbele katika utoaji huduma za afya kwa jamii inayotuzunguka.

# Mvua yabomoa nyumba, familia 10 zakosa makazi

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

FAMILIA zaidi ya 10 katika Kitongoji cha Myuyuda, Kata ya Sepuka, Wilaya ya Ikungi mkoani Singida zimekosa mahali pa kuishi baada ya mvua iliyoambatana na upepo kubomoa nyumba zao.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa kitongoji hicho, Jumanne Ighembe, alisema tukio hilo limetokea Februari 1, mwaka huu, limesababisha hasara ya zaidi ya Sh.milioni 59 kwa wakazi hao kutokana na uharibifu wa mali, mashamba na nyumba.

Ighembe aliwataja wanakijiji ambao nyumba zao zimeng'olewa bati ni pamoja na Shabani Kiseke, Shabani Jafari pamoja na Mussa Shabani.

Alisema wananchi wengine waliopata athari ni Batuli Juma ambaye nyumba yake imeng'olewa bati na vyombo vya ndani vikisobwa na Mwanahamisi Masimba ambaye paa la nyumba yake limeng'oka pamoja na mimea kuharibiwa shambani.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mnang'ana, Paskal Mdimi, alisema mashamba zaidi ya ekari 25 za mazao mbalimbali yameharibiwa.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Skelita Kagaruki, alisema gharama za nyumba zilizoharibiwa na kimbunga hicho ni zaidi ya Sh. milioni 50 na tathmini zaidi bado inaendelea kufanyika.

Diwani wa Kata ya Sepuka, Halima Ng'imba, alitoa pole kwa wananchi waliopatwa na mkasa wa nyumba zao kung'olewa na upepo na kuwataka kuwa na subira wakati serikali inaangalia namna ya kuwasaidia kutokana na janga hilo.



Wafanyabiashara wa makongoro, ulimi, mikia na vichwa vya ng'ombe wakiandaa bidhaa zao, wakati wakisubiri wateja katika soko la Mbuyuni, Kata ya Kizota, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waliosoma Sekondari Dodoma wakabidhi msaada wa kisima

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

UMOJA wa wanafunzi waliosoma Shule ya Sekondari Dodoma wamekabidhi msaada wa kisima cha maji walichochimba shuleni hapo kilichogharimu Sh. milioni 28.5 kama sehemu ya kutatua kero ya maji.

Katibu wa umoja huo wa wanafunzi waliomaliza shule kati ya mwaka 1970 hadi mwaka 1979 Mwanaharusi Lesso, alisema Julai 2023 walifanya ziara ya kutembelea shule hiyo, ndipo wakapokea kilio hicho kutoka kwa mkuu wa shule.

Lesso alisema jambo hilo liliwaumiza kwa kuwa katika kipindi chao hakukuwa na shida ya maji kutokana na idadi ndogo ya wanafunzi waliokuwapo wakati huo.

"Kwa pamoja tulisema hili tunalibeba na lazima tulifanye, tunashukuru leo limetimia kama tulivyotaka kwa hiyo wanafunzi wenzetu wa sasa wanakwenda kupata maji ya uhakika," alisema Lesso.

Akizungumza kwenye makabidhiano hayo, Mwenyekiti wa Bodi ya Shule hiyo, Dk. Kenneth Nzowa, alisema shule hiyo inakabiliwa na changamoto kubwa ya uhaba wa maji ambapo hupelekea mambo mengi kukwama.

Dk. Nzowa alisema kabla ya kuchimbwa kwa kisima hicho wamekuwa wakipata wakati mgumu hasa kwa wanafunzi wa bweni ambao mara nyingine walikosa maji ya kufulia, wakati mwingine walipaswa kusubiri uongozi wa shule ununue maji kwa wanaouza kwenye magari.

Alisema tatizo hilo limefikia mwisho na hakutakuwa na kisingizio kingine kutoka kwa wanafunzi kuhusu suala la maji ambayo watayatumia pia kwa shughuli za kilimo cha bustani wa kuwa wanalo eneo la kutosha.

Kwa upande wake Meja Jenerali Mstaafu, Salim Kijuu ambaye alikuwa mgeni rasmi, aliwaomba Watanzania kukumbuka walikotoka ili warudishe fadhila kwa ndugu zao, kwamba serikali haiwezi kufanya kila jambo ila kwa ushirikiano wa pamoja na wadau.

Meja Jenerali Kijuu alisema miaka ya 1970 wakati wanasoma hapo, idadi ya wanafunzi ilikuwa ni ndogo lakini hakukuwa na uharibifu wa mazingira hivyo walipata maji ya kutosha.

Alisema mambo yamebadilika, vyanzo vya maji havitoshelezi lakini ongezeko la wanafunzi pia ni mtihani mwingine.

Hivyo, aliwataka vijana kusoma kwa bidii na maarifa kwa kuwa hakuna wanachoweza kufaidi kama hawatakuwa na maarifa mapana na uelewa mzuri vichwani mwao.

Alisema: "Shule hii ilitulea na kutupa msingi hadi hapa tulipo, lakini tunatoa somo kwa wengine nao wakumbuke namna walivyolelewa walikotoka, waendelee, wakafanye kwa kadri ya uwezo wao, changamoto hazikosekani kila mahali, ila kuwe na utaratibu wa kujiweka tayari kukabiliana na changamoto hizo tukisaidiana na serikali".





# Madiwani wataka tafsiri ya udumavu, kimo cha mtu, akili

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

MADIWANI wa Halmashauri ya Mji Njombe, wameomba wataalam kuwapa tafsiri sahihi ya udumavu kwa maelezo kuwa hawaoni uhusiano kati ya kimo cha mtu na akili.

Ombi hilo liliibuka kwenye kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji Njombe katika robo ya pili ya mwaka wa fedha 2023/2024 kilichofanyika juzi wilayani hapa.

Diwani wa Kata ya Matola, Edwin Mwanzinga alisema siyo busara kuendelea kutumia kimo cha mtu kutafsiri udumavu huku akisisitiza kuwa kimo cha wananchi hakihusiani na udumavu.

"Hili neno udumavu tafsiri yake sina imani nayo ina mapungufu, sisi tatizo letu ambalo tunalifahamu mtusaidie kwa sababu tunaoana wenyewe, mtusaidie kutuletea mabinti kutoka Kanda ya Ziwa mtakuwa mmetusaidia tutakuwa tumepata kizazi kirefu," alisema Mwanzinga.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu, Ulrick Msemwa ambaye ni Diwani wa Kata ya Luponde alisema wataalam wa lishe katika halmashauri wanaendelea kuchakata tafsiri sahihi juu ya suala linalohusu kimo.

"Wataalamu wetu wanaendelea kuchakata kutafuta tafsiri sahihi ili kuepusha mgongano," alisema Msemwa.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Njombe, Filoteus Mligo alisema jambo hilo linachanganya kwa sababu kila mtu anatafsiri yake jambo ambalo linapaswa kutolewa majibu.

Akitolea ufafanuzi juu ya usahihi wa binadamu kuwa na hali ya udumavu katika umri wa chini ya miaka mitano, Katibu Tawala wa Wilaya ya Njombe, Aghata Mhaiki alisema itambulike kwamba udumavu unaanza tangu mzazi akiwa mjamzito na unaweza ukazuiliwa mpaka miaka miwili.



Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya Suma JKT, Kapteni Rosemary Katani akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kukabidhi vifaa vya kufanyia usafi kwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Jiji hilo, John Nchimbi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wavuvi Ziwa Nyasa wahofia maisha yao

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WAVUVI wanaofanya shughuli ndani ya Ziwa Nyasa katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya wamesema maisha yao yako hatarini kutokana na kutumia zana duni za uvuvi ikiwemo mitumbwi ya asili.

Wavuvi hao wametoa kilio hicho mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase alipotemebelea Kijiji cha Ikombe kwa ajili ya kukagua shughuli za maendeleo.

Wakizungumza kwenye fukwe za Ziwa Nyasa, baadhi ya wavuvi walisema maisha yao yako hatarini kutokana na zana duni wanazotumia kufanya shuguli zao za uvuvi.

Jonathan Mwamgunda ambaye ni mvuvi wa samaki ndani ya Ziwa Nyasa alisema mitumbwi ya asili wanayoitumia wavuvi wengi haiwezi kuhimili mawimbi makubwa yanayosababishwa na dhoruba kali pale ziwa hilo linapochafuka.

"Wavuvi wengi tunatumia mitumbwi ya asili kwenda kuvua samaki katikati ya ziwa, sasa upepo mkali unapovuma na kusababisha mawimbi makubwa, huwa tunakuwa kwenye hatari kubwa ya kuzama ziwani kutokana na mitumbi yetu kushindwa kuhimili mawimbi hayo," alisema Mwamgunda.

Aliiomba serikali kuwasaidia zana bora za uvuvi ikiwemo mitumbwi na nyavu za kisasa ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija na wakiwa katika mazingira salama.

"Uvuvi wetu ni wa kizamani sana, tunaiomba serikali kwanza itusaidie kutufundisha mbinu za kisasa za kuvua samaki na pia ituwezeshe kwa kutupatia zana bora ili tuweze kufanya shughuli zetu za uvuvi kwa tija," alisema Mwamgunda.

Kwa upande wake Nelson Mwakilambo ambaye pia ni mvuvi ndani ya ziwa hilo alisema kuwa uvuvi wanaoufanya ndani ya Ziwa Nyasa ni ule wa kuwawezesha kujikimu na sio kuwaletea maendeleo.

"Mbinu tunazozitumia kuvua samaki zinatuwezesha kupata samaki wa kujikimu tu maisha yetu, lakini hatuwezi kujikwamua kiuchumi kwa sababu hatupati samaki wengi kutokana na teknolojia pamoja na zana zetu tunazotumia ni duni mno," alisema Mwakilambo.

Diwani wa Kata ya Matema, Antony Mwamgunda alisema kuna umuhimu wa serikali kuwawezesha wavuvi wa ziwa hilo kwa kuwa na wao wanayo haki kama ilivyo kwa Watanzania wengine.

Akijibu hoja za wavuvi hao, Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase alisema serikali imeshaanza kufanya jitihada za kuwawezesha wavuvi katika maeneo mbalimbali nchini na kuwataka wavuvi hao wavute subira akidai kuwa serikali itawafikia.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameshaanza kugawa boti za kisasa kwa wavuvi katika maeneo mbalimbali nchini na kusema kuwa wavuvi wa Ziwa Nyasa nao wako kwenye ratiba ya mgawo.

# Suma JKT yakaa mguu sawa kuanza usafi Jiji la Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU chache baada ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Mbeya kutoa siku 14 kwa Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, John Nchimbi kumaliza tatizo la kuzagaa kwa taka ndani ya Jiji hilo, Kampuni ya Suma JKT ambayo imeingia kandarasi ya usafi imewasili na vifaa mbalimbali yakiwemo magari 11 kwa ajili ya kuanza kazi hiyo.

Kampuni hiyo iliwasili jijini hapa kwa ajili ya kuanza usafi kwenye kata tano za Tarafa ya Sisimba ambazo ndizo wameanza nazo kwenye mkataba.

Akikabidhi vifaa hivyo kwa Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya Suma JKT, Kapteni Rosemary Katani alisema baada ya kusaini mkataba walipatiwa muda wa mwezi mmoja kupeleka vifaa vya kufanyia kazi hiyo.

Alisema pamoja na kupewa muda huo lakini wamepeleka vifaa baada ya wiki tatu na tayari wameshaanza kazi ya kuzoa taka kwenye maeneo ambayo wamekubaliana kufanya kazi.

Alisema wameshaajiri vijana wa kutosha kwa ajili ya kufanya kazi hiyo kwa mujibu wa mkataba na kwamba watahakikisha wanafanya usafi kwa ufanisi wakishirikiana na wananchi pamoja na viongozi mbalimbali wa serikali.

"Tunaahidi kufanya kazi hii kwa ufanisi mkubwa kwa sababu tuna vifaa vya kutosha kwa ajili ya kufanya kazi hii, tunachoomba kwa wananchi ni ushirikiano hasa wakati wa kukusanya kodi ya taka," alisema Kapteni Rosemary.

Alisema kampuni hiyo inafanya kazi ya usafi kwenye maeneo mbalimbali nchini na kwamba Jiji la Mbeya ni miongoni mwa maeneo hayo na kwamba wameanza na kata hizo tano lakini kadri siku zinavyokwenda wataomba na kata zingine.

Akipokea magari hayo, Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya Nchimbi alisema Jiji hilo lina kata 36 lakini wameanza na kata hizo tano ambazo ndizo kubwa zaidi na zina watu wengi kuliko maeneo mengine na hivyo hata kiwango cha uzalishaji wa taka ni kikubwa zaidi.

Alisema baada ya kuona ufanisi wa kampuni hiyo wataongeza kata zingine na itakapobainika kuwa uwezo wa kampuni ni mkubwa watapatia kazi kwenye kata zote ili usafi ufanyike kwa kiwango kinachofanana maeneo yote.

Alisema kampuni hiyo ndiyo iliyoonyesha uwezo mkubwa kwa kuwa na idadi kubwa ya magari na wafanyakazi wengi ambao wanaweza wakafanya kazi kwa haraka zaidi.

Alisema Jiji la Mbeya ndilo lenye ada ndogo ya taka ikilinganishwa na mikoa mingine kwa maelezo kuwa ada yao ni Sh. 2,000.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Iyela, Mercy Mwakalinga alisema kata yake ni miongoni mwa kata kubwa ambazo zimekuwa zikikabiliwa na tatizo la uchafu wa mazingira na kwamba kwa sasa ana imani tatizo hilo litakwisha.





## Upotevu wa mapato ya bahari wamshtua waziri, atoa agizo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Zanzibar (ZAECA) imetakiwa kufanya uchunguzi wa kina dhidi ya wafanyakazi wa mkataba waliokuwa wanaohusika na ukusanyaji wa mapato katika hifadhi za bahari (CHABAMCA), kutokana na kupotea kwa mapato katika maeneo hayo.

Maeneo hayo yaliokuwa na opotevu mkubwa wa mapato ni pamoja na Kituo cha Hifadhi ya Jitini, Mizingani, Forodha Mchanga, Africa House na Prison Island.

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Shaabani Ali Othman, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wakuu wa taasisi wa wizara hiyo.

Alisema licha ya wizara kuwaamini vijana hao kwa kuwapa maeneo nyeti ya ukusanyaji mapato lakini kunadalili za upotevu wa mapato, hivyo aliitaka mamlaka hiyo kufanya uchunguzi wa kina kubaini kasoro zilizojitokeza katika maeneo hayo.

"Nakuagiza fanya uchunguzi wa kina bila kumuonea mtu na kama wanamakosa wachukuliwe hatua za kisheria" alisema.

Kadhalika alitumia nafasi hiyo kuwataka wakuu wa taasisi kuajiri vijana wengine hadi wizara itakapokamilisha kazi ya kutafuta wafanyakazi wa kudumu katika maeneo hayo.

Mkurugenzi wa Uchunguzi na Operesheni wa ZAECA, Nassor Ahmed Haji alisema atahakikisha anafanya uchunguzi wa kutosha juu ya tuhuma hizo na aliyehusika atachukuliwa hatua za kisheria.

Wafanyakazi hao wamesimamishwa kazi kufuatia Waziri wa Wizara hiyo kufanya ziara ya kushtukiza na kubaini kupotea kwa mapato kutoka na kuingia wageni bila kufanya malipo.

# Watoa maoni kuhusu uraia pacha, katika matumizi ya teknolojia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WADAU walioshiriki kongamano la kujadili sera ya mambo ya nje visiwani Zanzibar, wamezungumzia ushiriki wa wanawake kwenye ubalozi, suala la uraia pacha na kutanua wigo katika matumizi ya teknolojia kwa ajili ya kukuza biashara nje ya nchi.

Akizungumza katika kongamano hilo lilofanyika juzi visiwani hapa, Mwenyekiti wa Chama cha ADC, Hamad Rashid Muhammed alisema bado suala ya usawa wa kijinsia halijazingatiwa katika nafasi za ubalozi na hivyo ushiriki wa wanawake ni mdogo ikilinganishwa na wanaume.

"Wizara ya Mambo ya Nje bado haijawa na usawa wa kijinsia katika nafasi zake za uongozi kwa mabalozi wanaoiwakilisha nchi, ni vizuri katika sera hili nalo likazingatiwa, juzi kwenye vyama vya siasa tumeambiwa angalau dawati la wanawake lisipunguwe asilimia 30 sioni kwanini katika mazingira mengine wanawake wasipate nafasi" alisema Hamad.

Aidha alisema upungufu mwingine ni kuna mambo ambayo yameachwa katika sera ya mambo ya nje, ikiwemo nafasi ya Rais wa Zanzibar anapokwenda nje ya nchi.

Hamad alisema kuna wafanyabiashara Watanzania ambao huenda kufanya biashara nje ya nchi lakini huwa hawapati ulinzi na wanapopata matatizo huwa hawapati msaada wowote hivyo ni vyema katika sera mpya ya mambo ya nje lazima iwatambue na iwalinde.

Akizungumzia kuhusu deni la taifa, alisema suala la mfumo wa fedha duniani umebadilika, lakini Tanzania imebaki katika utaratibu wa zamani, hivyo ni vyema na hilo kufanyiwa kazi.

Naye Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu Zanzibar, Ussi Khamis Debe, alisema lazima sera izingatie mahitaji ya watu wenye ulemavu kwa sababu bado hawajazingatiwa.

Alisema sera ya mambo ya nje ambayo inafanyiwa maboresho katika masuala ya watu wenye ulemavu wanatemea zaidi Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu wa mwaka 2006 na Tanzania imeridhia kutekeleza.

Alisema lakini katika mkataba huo kuna vitu havijazingatiwa katika Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001.

Aidha alisema takwimu za watu wenye ulemavu duniani kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Afya Duniani imeonesha kuwa kuna watu wenye ulemavu tofauti bilioni 1.3 sawa na asilimia 16 ya idadi ya watu duniani na Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 asilimia 10.4 ya watu wa Zanzibar wana ulemavu.

Alisema kuna haja ya kuzingatiwa kundi hilo la watu wenye ulemavu licha ya jithada zianzofanywa na marais Dk. Samia Suluhu Hassan na Dk. Ali Hassan Mwinyi.

Katibu Tawala Mkoa wa Kusini Unguja, Radhia Khatib Haroub, alipongeza kuwepo kwa msisitizo wa kulinda desturi na utamaduni katika sera hiyo ya mambo ya nje.

Akizungumza kuhusu, amani ulinzi na usalama alishauri katika sera hiyo kuwepo kwa mpango mkakati wa ulinzi na usalama ili kudhibiti uhalifu wa kuvuka mipaka.

Aidha alishauri katika sera hiyo pia kuwe na udhibiti wa matumizi ya mtandao, ambapo eneo moja ambalo utamaduni wa Tanzania unaathiriwa ni katika matumizi yasio sahihi ya kimtandao.




Mganga Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani, Kandi Lussingu (katikati), akizungumza katika uzinduzi wa mradi wa kuimarisha upatikanaji wa haki na huduma nyingine za kijamii kupitia huduma za msaada wa kisheria na ushirikiano kwa jamii na waraibu wa dawa za kulevya, unaoratibiwa na shirika lisilo la kiserikali la Life & Hope Rehabilitation Organisation (LHRO), wilayani humo jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo, Al-Karim Bhanji na Mwakilishi wa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Mwambao, Hapsa Juma. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wizara ya Ardhi yatoa elimu ya uthamini wa fidia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Dk. Mngereza Mzee Miraji, amesema Wizara ya Ardhi imeanza kutoa elimu kwa wadau ili kuwajengea uwelewa wa muongozo wa uthamini wa fidia kwa wananchi.

Dk. Mngereza aliyasema hayo jana wakati akizungumza na masheha wa Wilaya ya Mjini na Wilaya ya Magharibi "A" Unguja.

Alisema wizara kupitia Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imeandaa muongozo maalum wenye kubanisha mchakato wa uthamini, lengo likiwa kuimarisha huduma bora wanazozitoa kwa wananchi.

Aidha alisema kutokana miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya ujenzi wa bandari, barabara pamoja na Uwanja wa Ndege wa Pemba serikali imeona ipo haja kuanda muongozo sambamba na kuwafikishia wananchi elimu ili wafahamu haki na stahiki zao.

Naye Mthamini Mkuu wa Serikali, Tahir Mussa Omar alisema kuwa wakati wa utekelezaji wa miradi tofauti ya serikali kumekuwa kukijotekeza changamoto nyingi kwa wananchi juu ya upatikanaji wa stahiki zao jambo ambalo huleta migogoro isiokuwa ya lazima.

Tahir alisema Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kupitia Wizara ya Ardhi imeamua kuja na muongozo huo wa uthamini wa fidia ili kuondosha changamoto hizo na badala yake uwasaide wananchi kupata haki zao kwa wakati.

Aidha alisema muongozo huo ulioandaliwa umekuja na pendekezo la muda maalum ambalo wananchi wanapaswa kulipwa fidia zao baada ya kufanyiwa tathmini kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja tofauti na utaratibu ulivyokuwa awali.

Wakitoa michango yao masheha waliupongeza uongozi wa Wizara ya Ardhi kwa kuwapatia elimu hiyo kwani itasaidia kuondoa changamoto zinazojitokeza katika maeneo yao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**LOVENESS ANOLD MASIMBA,** Anatangaza kupotea kwa Cheti Cha Kidato cha Nne Chenye Index no **S.1602/0014** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Sekondari Kisukuru Regent Mwaka **2007.** Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI: **REF:BUG/W/A.16/14/VOL.XXI/.60**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**INTERNATIONAL COMMITTEE OF THE RED CROSS** inatangaza kupotea kwa kadi za gari aina ya **TOYOTA** zenye usajili namba **T 260 CD38 NA T260 CD37 , CHASSIS NAMBA: JTERB71700F001773 NA JTEEB71570F002028** na **ENGINE NAMBA: 1HZ0920289 na 1HZ0915654.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/ILA/15054/2024**

## TANGAZO

**MIMI NDUGU DANFORD GAMBALIKO** NAMTAFUTA NDUGU **EDMUND EDWARD URIO** ALIYENIUZIA KIWANJA **PLOT NO. 827 BLOCK G TEGETA MASAITI.** UPATAPO TANGAZO HILI NITAFUTE KWA NAMBA HII **0738261460**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JEREMIA DAUDI JOAKIM** Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki(HAOJUE) yenye namba za usajili MC 419BVJ, Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nayeye.

**PHQ/MOR/MOR/2250/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJ

**NAFTAL RASHID KIHWELO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA **BAJAJ** YENYE USAJILI **MC810 ARH** AINA YA TVS RANGI YA KIJANI ,YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI JALADA NAMBA **PHQ/IRI/IRI/1467/2024.**

---

**MAHAKAMA KUU TANZANIA ARUSHA**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NAMBARI 31 YA MWAKA 2023**
**BARUA YA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YA**
**BETHUEL ELIA LYIMO..................MAREHEMU**
**NA**
**ANNETTE BETHUEL LYIMO**
**EVELYN BETHUEL LYIMO...............WAOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI YA 75).**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia maombi haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji waliotajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 25 mwezi wa Machi, mwaka wa 2024.

Imewasilishwa Arusha leo tarehe 13 Mwezi wa Didemba mwaka 2023.

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU**
**ARUSHA.**

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
ARUSHA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya KINONDONI**
**Kituo cha KINONDONI**
**Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Madai/ Ndoa Na.95/2023**

**Jina la mdai.......................................GLORIA KIMARO**

**Jina la mdaiwa..................................SARAH ZABLON**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**

**(kanuni ya 62 ya kanuni za uendeshaji mashauri Mahakama za mwanzo)**

KWA **SARAH ZABLON KWAMBA** Mdai ameleta maombi mbele ya mahakama hii kwaajili ya utekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu. Unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii tarehe 8 mwezi 02 mwaka 2024 kueleza kwanini Hukumu isitekelezwe dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa mahakama leo tarehe 31 mwezi 01 mwaka 2024

PRIMARY COURT KINONDONI DAR ES SALAAM * TANZANIA *

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KINONDONI
WILAYA YA KINONDONI

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA DISTRICT**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 1834 of 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**JOSEPH SEBASTIAN PANDE**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR GRANT OF**
**LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**JANE DAMIAN KULWA.**

**GENERAL CITATION**
**RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **5 day of MARCH...2024**
Dated at Dodoma this 2 day of **FEBRUARY...2024**

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT

..............................................................
**REGISTRY OFFICER**

---

**Summons to appear (O.V, R.20(1) of ( Civil Procedure Code)**
**(substituted service)**

**IN THE COURT OF TANZANIA DAR ES SALAAM**
**(LAND DIVISION)**

**TAXATION 26212 OF 2023**

**GLORIA IRIRA....................................................D/HOLDER**

**VERSUS**

**SUDI MRISHO NGWABI & ANOTHER........................DEBTOR**

**TO: ASHOK BHAILAL SHANGHAVI**
**DAR-ES-SALAAM**

**WHEREAS:** the above named D/HOLDER obtained an EXECUTION CAUSE against you. You are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or authorized Agent on 6th day MARCH, 2024 at 09:00 AM before HON. M.LUKINDO, DR
To answer the said EXECUTION and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your replay.
**TAKE NOTICE** that, in default of your appearance on that day, the said EXECUTION will be heard and determined in your absence.
Given under my hand and the seal of this Court, this 5th MARCH 2024.

Seal of this Court
LAND DIVISION

..............................
**DEPUTY REGISTRAR**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No 1153 of 2024**

**In the matter of the estate of the late JANETH CEPHER CHIRIMI of Ntyuka within Dodoma City**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by CEPHER JAPHET CHIRIMI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN NO. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 15 day of 2 ...................... 2024

Dated at Dodoma this 23 day of 1................2024

COURT SEAL
DODOMA DISTRICT

..............................
RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA ILEMELA**
**MWANZA**

**SHAURI LA NDOA NAMBA 10 LA 2023**

**IBRAHIM SAMWEL MATEREGO............MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**KHIMI BITON KYANDO.......................MJIBU MAOMBI**

**KWA: KHIMI BITON KYANDO POPOTE ULIPO**

UNAFAHAMISHWA KWAMBA MLETA MAOMBI HAPO JUU AMELETA SHAURI DHIDI YAKO NA LIMEPANGWA KUTAJWA TAREHE 08/02/2024 SAA 03:00 ASUBUHI MBELE YA MHE. A.N. SUMARI - RM KWA HIVYO UNATAKIWA KUHUDHURIA MAHAKAMANI SIKU HIYO WEWE WENYEWE , WAKILI WAKO AU MTU MWINGINE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUJIBU SHAURI HILO.

KAA- UKIJUA KUSHINDWA KUFIKA SHAURI HILO LITASIKILIZWA NA KUTOA UAMUZI BILA WEWE KUWEPO.

IMETOLEWA NAMI KWA AMRI NA CHAPA YA MAHAKAMA LEO TAREHE 31/01/2024.

**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA ILEMELA**

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA**
**AT DAR ES SALAAM**

**CIVIL APPEAL NO.292 OF 2023**

**JUSTINE F. BUFURE ............................APPELLANT**

**VERSUS**

**HAJI R.MWIKALO...............................1st RESPONDENT**
**JACK PEMBA ..................................2nd RESPONDENT**

**TO: JACK PEMBA**

**"WHEREVER YOU ARE"**

**TAKE NOTICE** that the hearing of this Appeal will take place at Dar Es Salaam on 14th day of February, 2024 at 09:00am.
If no appearance is made on your behalf by yourself, your pleader or by someone authorized by law to act for you in this Appeal, it will be heard and decided in your absence.
Given under my hand and the seal of the Court this 19th day of January, 2024.

THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA

A. S. CHUGULU
**For: REGISTRAR**
**COURT OF APPEAL**

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF**
**MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 1836 OF 2024**
**In the Matter of the Estate of the Late:**
**RECHO IBRAHIM MJEMA**

**By 1: IBRAHIM YEREMIA MJEMA.**
**2: ________________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the M. KALOMO day of 12/02/2024
Dated at 02 day of 02/2024

..............................
RESIDENT MAGISTRATE

---


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,
KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Mfalme Charles agunduliwa kuwa na saratani

**LONDON,** UINGEREZA

KASRI la Burkingham limesema kuwa Mfalme wa Uingereza, Charles III, amegunduliwa kuwa na ugonjwa wa saratani na ameanza matibabu bila kutoa maelezo zaidi kuhusu aina ya saratani aliyonayo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kasri ya Buckingham, Mfalme Charles mwenye umri wa miaka 75 atasitisha majukumu yake ya umma, lakini ataendelea na shughuli za serikali na hatakabidhi majukumu yake ya kikatiba kama mkuu wa taifa kwa yoyote.

Taarifa hiyo ilisema Mfalme Charles alipimwa na kupatikana na ugonjwa huo wakati alipolazwa hospitali kwa siku tatu mwezi uliopita kwa matibabu ya tezi dume.

Pia ilieleza kuwa vipimo alivyofanyiwa Mfalme akiwa hospitali kutibiwa tezi dume, ndio vilibaini ugonjwa huo lakini haikutoa maelezo yoyote kuhusu aina ya saratani iliyogunduliwa, na kwamba muda mfupi baada ya kugunduliwa na ugonjwa huo, Mfalme Charles alianza kupata matibabu akiwa nyumbani.

"Mfalme amechagua kuweka wazi hali yake ya afya ili kuepusha uvumi na kwa matumaini kwamba, kufanya hivyo kutasaidia umma kuelewa zaidi ugonjwa huo na wale wote duniani ambao wameathiriwa na saratani," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Aidha, Waziri Mkuu wa Uingereza, Rishi Sunak, alimtakia Mfalme Charles afueni kamili na ya haraka "Sina shaka kuwa atarejelea afya kamili baada ya muda mfupi na najua nchi nzima itakuwa ikimtakia heri," alisema. **VOA**

# Simai ahojiwa kamati ya maadili CCM

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Mohamed Said, ameitwa kuhojiwa na Kamati ya Maadili ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Jimbo la Tunguu ikiwa ni takriban wiki mbili tangu kujiuzulu wadhifa huo.

Simai alihojiwa jana katika tawi la CCM Tunguu majira ya 4:00 asubuhi na wajumbe wa Kamati ya Maadili wakiongozwa na Mwenyekiti wa Tawi, Mtumwa Ali Mgeni.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa baadhi ya wajumbe, Simai amehojiwa kutokana na utaratibu alioutumia kujiuzulu uwaziri pamoja na kumjibu Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, alipoeleza sababu za kujiuzulu waziri huyo.

"Sikutarajia kukuta waandishi wa habari. Hiki ni kikao cha kawaida lakini mimi si mzungumzaji wa kilichozungumzwa. Msemaji ni mwenyekiti na katibu wa tawi hili, watafuteni wao ndio wasemaji," alisema Simai baada ya kutoka kwenye kikao hicho baada ya kufuatwa na waandishi .

Simai alipotangaza kujiuzulu, alisema ameamua kuchukua uamuzi huo kutokana na mazingira ya kazi kutokuwa rafiki, siku chache baada ya kujitokeza uhaba wa pombe Zanzibar na kuathiri maendeleo ya sekta ya utalii visiwani humo.

Uhaba huo umesababishwa na Bodi ya Udhibiti wa Vileo Zanzibar baada ya kuzinyima kampuni tatu zenye uzoefu wa uingizaji pombe kwa zaidi ya miaka 30 na kuzipa kampuni mpya tatu ambazo zinalalamikiwa kutokuwa na sifa wala uwezo.

Kwa mujibu wa taarifa za ndani, Simai alipokea taarifa ya kutakiwa kufika ofisi za CCM Jimbo saa 3:00 asubuhi kuhudhuria kikao cha kamati ya maadili.

Kuhojiwa kwa Simai kumeibua mjadala mkubwa kwa wanachama wa CCM kwa vile hawajui hatima yake ikiwamo ya uanachama wa CCM na uwakilishi wa Jimbo la Tunguu ambalo ni Mwakilishi katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Taarifa kutoka ndani ya CCM zinadai kuwa huenda kufika kwake katika kikao hicho cha maadili ni hatua ya mwanzo katika kuamua hatima yake ndani ya CCM na uwakilishi wake katika Baraza la Wawakilishi.

Hiyo pia inatokana na historia kuonyesha kuwa baadhi ya wanachama na mawaziri waliowahi kuitwa kwenye kamati kama hiyo, walifukuzwa uanachama.

Miongoni mwa waliokumbwa na hatua ya kufukuzwa uanachama ndani ya CCM Zanzibar baada ya kufikishwa kwenye kamati hiyo ni aliyekuwa Mwakilishi wa Jang'ombe, Abdallah Diwani; aliyekuwa Waziri wa Maji, Ardhi na Nishati, Mansour Yussuf Himid, mwanasiasa mkongwe na mtoto wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Balozi Ali Karume na mwanasiasa maarufu Zanzibar na mtoto wa Waziri Mkuu wa Kwanza wa Zanzibar, Baraka Mohamed Shamte.

Kabla ya wanachama na viongozi hao kufukuzwa, wanasiasa mashuhuri na waliowahi kushika nafasi nyeti serikali waliofukuzwa na hatimaye kuanzisha Chama Cha Wananchi (CUF) ni Waziri Kiongozi wa zamani, Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Jaji Mkuu wa Zanzibar, Ali Haji Pandu, wanasiasa wakongwe Shaaban Ali Mloo, Hamad Rashid Mohamed na aliyekuwa Naibu Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa Zanzibar, Khatib Hassan.



Baadhi ya wafanyabiashara wakikusanya baadhi ya mabaki ya vitu baada ya Soko Kuu la Mbuyuni kuteketea kwa moto katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro usiku wa kuamkia jana na kuteketeza vibanda 2000. **PICHA: MARY MOSHA**

# Moto ulivyoteketeza mali za zaidi wafanyabiashara 2000

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KUKOSEKANA kwa gari la Zimamoto Mkoa wa Kilimanjaro, kumetajwa kuwa chanzo kwa wafanyabiashara zaidi ya 2,000 wa soko kuu la matunda na mboga la Mbuyuni liliko Manispaa ya Moshi mkoani humo, kupoteza mali zao baada ya moto kuzuka majira ya sita usiku wa kuamkia Februari 6.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya mashuhuda wa tukio hilo, Emmanuel Urio alisema baada ya moto kutokea tatizo la upatikanaji wa gari la zimamoto limesababisha wafanyabiashara kushindwa kuokoa vitu vyao.

"Hii sio mara ya kwanza moto kutokea eneo hili, kila siku gari la Zimamoto ni bovu, lakini watendaji wa jeshi hilo kila mara hupita kwenye maduka na kuchukua fedha Sh. 40,000 kwa ajili ya matengenezo na kuboresha huduma ya dharura ila inapotokea tatizo hawakosi sababu, hili tatizo kubwa kwa mkoa," alilalamika Elizeth Mrema.

Baadhi ya wafanyabiashara waliopata madhila hayo, akiwamo Mwanahawa Mvungi, alisema baada ya kufika katika eneo hilo, moto ulikuwa umeteketeza takribani vibanda 10 licha ya moto huo kusambaa kwa kasi kutokana na upepo.

"Moto umetokea majira ya 12:09 mimi nilifika12:15 ila gari la zimamoto lilimefika 02:50 ingawa viongozi wengi walikuwa eneo la tukio, hii inasikitisha na kukatisha tamaa. Viongozi wanafika na kuwa sehemu ya tatizo badala ya kuwa sehemu ya suluhishi," alisema Mwanahawa.

"Tumepokea maelekezo kutoka kwa Mkuu wa mkoa ya kurejesha miundombinu iliyokuwapo na leo (jana) Februari 6, Baraza la Madiwani litakaa na kujadili kuona namna ya kutekeleza agizo hilo," alisema Meya wa Manispaa ya Moshi, Zuberi Kidumo.

Mwenyekiti wa soko hilo, Lameck Mzirai, alisema uchunguzi wa awali unaonyesha wafanyabiashara zaidi ya 2,000 wamepoteza mali zao zote kati ya 2,500 katika eneo hilo.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto Mkoa wa Kilimanjaro, Jeremea Mkomagi, alisema majira 12:34 usiku wa kuamkia Februari 6, mwaka huu, walipokea taarifa ya kuungua kwa soko la Mbuyuni na askari walifika eneo la tukio na kudhibiti kusambaa kwa moto huo.

"Ila gari lilichelewa kidogo kwa kuwa lilikuwa linatokea katika Kiwanda cha Sukari cha TPC, hadi sasa moto umezima kwa asilimia 95 kwa sasa kilichobakia ni kusawazisha," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro, Nurdini Babu, alisema moto ulizuka majira ya 12:00 usiku na timu mbalimbali zilishirikiana kuuzima licha ya kukabiliwa na tatizo la ubovu wa gari la zima moto. "Nimeona wananchi wanarusha lawama kwa Jeshi la Zimamoto ila nawaomba wananchi kuwa majanga kama haya hayapangwi kwa kuwa wakati mwingine na sisi tunakuwa hatujajipanga, lakini niwashukuru wote waliojitokeza kuwasaidia wenzao kuokoa mali zao, pia natoa onyo kwa baadhi ya vijana wanaotumia matukio kama haya kufanya uhalifu kwa kuwa hatutawavumilia," alisema.

# MUDATHIR HATARI AKITOKEA BENCHI, AFUNGUKIA BAO LAKE

**Adam Fungamwango na Oliver Albert**

KWA mara nyingine tena, kiungo wa Yanga, Mudathir Yahaya juzi alifunga bao pekee dhidi ya Dodoma Jiji akitokea benchi, huku akikiri anakuwa hatari zaidi akiingia kipindi cha pili kwani anakuwa amepata maelekezo maalum kutoka kwa Kocha Mkuu, Miguel Gamondi.

Mudathir, aliingia dakika ya 62 kuchukua nafasi ya Jonas Mkude na dakika ya 86 akaweka mpira ndani ya wavu, akipata krosi pasi kutoka kwa beki wa kushoto, Nickson Kibabage na kuwa bao pekee lililoipa Yanga ushindi wa 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji, mechi ikichezwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

Mchezaji huyo alirudia tena alichokifanya Septemba 30, mwaka jana katika mechi ya Ligi Kuu, alipoifungia Yanga bao pekee dhidi ya Namungo, pia akitokea benchi.

Katika mechi hiyo, aliingia dakika ya 68 kuchukua nafasi ya Pacome Zouzoua, na dakika mbili kabla ya mechi kumalizika akapachika bao akiunganisha krosi kutoka kwa beki wa kulia, Yao Kouassi.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, kumalizika alisema siri ya kuwa ni hatari zaidi anapoingia kipindi cha pili ni maelekezo maalum anayoyapata kutoka kwa kocha wake, Gamondi.

„Katika mechi hii mwalimu aliniambia uningia ili kwenda kumsaidia kiungo mkabaji mwenzangu nafasi hiyo iwe na watu wawili, lakini akaniambia mimi niwe nakwenda mbele kusaidia mashambulizi na kurudi mara moja kumsaidia mwenzangu, katika nyendo zangu nikaipata moja imewekwa pale kwenye boksi, nikaitumia," alisema Mudathir.

Baada ya kufunga bao hilo, Mudathir alitoa kizuia ugoko(Shin guard) na kuonyesha kama ishara ya kupiga simu huku mwenyewe akisema alikuwa akiwapigia simu mke na mtoto wake kuwa „mmeona nilichowaambia"

Kiungo huyo kabla ya mechi alitabiri kuwa angefunga kwani hajafunga siku nyingi na kweli maneno yake yakatimia.

„Nilipoingia nilikuwa na lengo moja tu la kuisaidia timu yangu kushinda na nikapambana kupata bao na nashukuru Mungu nikafunga na tukapata ushindi.

„Ndio maana baada ya kufunga nikawa kama napiga simu kumwambia mke wangu na mwanangu kuwa mmeona nilichowaambia kabla ya mechi kuwa nikiingia tu lazima nifunge, „alisema Mudathir.

Mudathir alisema anafurahi kuona wamepata ushindi uliowarudisha kileleni kwenye msimamo wa ligi hiyo akiamini kuwa hawatatoka tena kwenye hiyo nafasi.

„Nafurahi tumerudi kileleni na naamini tutaendelea kuwa hapo juu kwa muda mrefu muhimu ni kuhakikisha tunafanya vizuri katika michezo mingine ijayo," alisema.

Yanga itashuka tena uwanjani kesho kukabili Mashujaa FC kwenye mchezo utakaopigwa Uwanja wa Azam Complex.

MILIKI...




Beki wa kulia wa Yanga, Kouassi Attohoula Yao, akimiliki mpira dhidi ya mchezaji wa Dodoma Jiji FC, Habib Rajab, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi na Yanga kuibuka na ushindi wa bao 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

# Tamasha kubwa la utulivu lazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Utulivu Space, inatarajia kufanya tamasha kubwa liitwalo 'Utulivu Experience', lenye lengo la kuusherehekea Utaifa wa Mtanzania kutokana na amani na utulivu uliopo nchini.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, rais wa taasisi hiyo, Ibrahim Rwegerera, alisema wameamua kuja na tamasha hilo lengo likiwa ni kuwakutanisha watu mbalimbali waliochangia kuwapo wa amani na utulivu uliopo nchini.

Alisema tamasha hilo litakua la kwanza kufanyika katika mazingira ya kitulivu ambapo litawakutanisha watu mbalimbali wakiwamo watu maarufu ambao wanaasili ya Kitanzania watakaa na kujadilina na kunywa chai pamoja.

"Tamasha hili linawahusu watu wote wenye asili ya Kitanzania, tunawakaribisha wote wacheza mpira, wasanii, wanasiasa na kila mwenye asili ya Kitanzania maana hii itakua ni siku yetu ya kusherehekea Utanzania wetu hivyo tujitokeze kwa wingi hili litakua tamasha la kihistoria,"alisema.

Alisema tamasha hilo litafanyika kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza linatarajiwa kufanyika Aprili 20, mwaka huu katika ukumbi wa Super dom Masaki na awamu ya pili litafanyika Zanzibar mwishoni mwa Novemba mwaka huu.

Kwa upande wa mmoja wa waandaaji wa tamasha hilo, Anthony Luvanda, alisema linatoa fursa kwa wageni kuja kujifunza asili ya Mtanzania ikiwamo ukarimu na utamaduni wake.

"Nitoe wito kwa watu wa mataifa yote kuja kujifunza asili yetu lugha yetu, mavazi yetu ukarimu na utulivu wetu, waje wajifunze utamaduni wa Kiswahili,"alisema Luvanda.

Aidha, Luvanda aliongeza kuwa utulivu unaanzia kwa mtu binafsi, lakini unachochewa na amani iliyopo katika nchi hii.

Tamasha la Utulivu Experience litafanyika Aprili 20, jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa Super dom Masaki na litapambwa na wasanii wakiwamo wazamani na watu waliochangia amani na utulivu uliopo nchini.

## Singida FG kuisaidia Yanga kwa Kagera

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Singida Fountain Gate FC, Thambo Senong, amesema kama Yanga walishindwa kupata pointi tatu dhidi ya Kagera Sugar, basi wao watakwenda kuzichukua Februari 12, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Senong alisema kikosi chake kimefika Mwanza na wanazipigia mahesabu makali pointi tatu za Kagera Sugar ambazo ni muhimu kuelekea katika azma yao ya kumaliza nafasi nne za juu, hivyo wanaendelea kujiandaa kwa mchezo huo kwa kuhakikisha wanavuna alama zote tatu.

Alisema kulingana na wachezaji aliobakia nao kwa sasa, wanaenda kufanya vizuri, lakini kurejea kwa baadhi ya nyota wao wa kimataifa akiwamo Enecko Atta na Nicholas Gyan waliokuwa majeruhi, kunazidi kuwaimarisha.

"Kulingana na wachezaji niliokuwa nao kwa sasa matarajio yangu makubwa tunaenda kufanya vizuri katika mchezo huu pamoja na michezo iliyopo mbele yetu kwa sasa tunahitaji alama muhimu dhidi ya Kagera Sugar," alisema Thambo.

## Washindi 20 Airtel wakabidhiwa zawadi

**Na Maulid Mmbaga**

KAMPUNI ya simu ya Airtel imetoa zawadi kwa wateja wake zaidi ya 20 kwa nyakati tofauti, walizoshinda kwenye Kampeni ya 'Upige Mwingi' ambayo mwishoni washindi watapelekwa Ivory Coast kuangalia mechi ya fainali ya Mataifa ya Afrika (Afcon).

Akizungumza Dar es Salaam jana, wakati wa hafla ya ugawaji wa zawadi hizo zikiwamo mipira, simu na televisheni, Meneja Uhusiano wa Airtel, Jennifer Mbuya, alisema lengo la droo hiyo pia ni pamoja na kuiwezesha jamii kupata vifaa vitakavyowasaidia katika kuendesha shughuli za kujiingizia kipato kama pikipiki, bajaji na simu.

Alisema kampeni hiyo ilianza Januari mwaka huu na itaendeshwa kwa siku 90 katika kipindi hiki cha kuelekea mechi ya fainali ya AFCON, akisisitiza kuwa kila mmoja anaweza kushiriki huku akitoa wito kwa Watanzania kuepuka matapeli ambao watawapigia simu na namba tofauti na 100 na kudai wameshinda.

"Mwanzo tulisisitiza kwamba tutakuwa na washindi ambao tutaenda nao AFCON na sasa washiriki wamekuwa ni wengi na mwisho wa wiki hii tunatarajia kwenda Ivory Coast, natumai wengi wanaangalia michezo hii imekuwa na ushindani mkubwa sana, tunaona uwezo wa Afrika, endeleeni kutumia huduma zetu twende pamoja," alisema Jennifer.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### POCHETTINO HATIMULIWI

KOCHA wa Chelsea, Mauricio Pochettino kwa sasa hayuko kwenye hatari ya kutimuliwa licha ya timu yake kupata msururu wa matokeo mabaya. **(Telegraph)**

### VARANE KUMFUATA CR7

KLABU ya Ligi Kuu Saudi Arabia, Al-Nassr inataka kumuunganisha tena beki wa Manchester United, Mfaransa Raphael Varane mwenye umri wa miaka 30, na mchezaji mwenzake wa zamani wa Real Madrid, Cristiano Ronaldo. **(Star)**

### SANCHO MILIONI 50

MANCHESTER United inataka ada ya kati ya pauni milioni 40 na milioni 50 kwa winga wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo katika klabu yake ya zamani ya Borussia Dortmund. **(Football Insider)**

### SAVIO HUYOOO CITY

KLABU ya Manchester City imekubali dili la kumsajili winga Savio mwenye umri wa miaka 19. Mbrazil huyo kwa sasa yuko kwa mkopo Girona kutoka Troyes. **(Fabrizio Romano)**

### SPURS YAMTAKA RAPHINHA

KLABU ya Tottenham Hotspur inavutiwa na mshambuliaji wa Barcelona na Brazil, Raphinha, 27. **(Paul O'Keefe)**

### MBAPPE MSHAHARA BADO

REAL Madrid bado haijakubaliana mshahara na mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 25. **(Independent)**

### CHERKI MSIMU WA JOTO

FULHAM itafanya jaribio la pili kumsajili kiungo mshambuliaji wa Lyon na Ufaransa, Rayan Cherki mwenye umri wa miaka 20, msimu wa majira ya joto baada ya kushindwa kwa ofa ya pauni milioni 35 Januari. **(Sun)**

### BAILEY ATAKIWA VILLA

ASTON Villa imefikia makubaliano ya mdomo na Leon Bailey ambaye ni winga wa Jamaica mwenye umri wa miaka 26 ili kusaini mkataba mpya wa muda mrefu na klabu hiyo. **(Telegraph)**

### DECO AMKATAA KLOPP

MKURUGENZI wa Michezo wa Barcelona, Deco, amesema kuwa si „wakati muafaka" kuzungumza kuhusu kocha anayeondoka Liverpool, Jurgen Klopp, kama mrithi anayeweza kuchukua mikoba ya Xavi pale Camp Nou. **(La Vanguarda via Metro)**

### FLICK AITAKA BARCELONA

KOCHA wa zamani wa Ujerumani na Bayern Munich, Hansi Flick anajifunza Kihispania na angependa kuchukua mikoba ya kuinoa Barcelona msimu wa majira ya joto. **(Bild)**

### UI-JO AKUBALI

MSHAMBULIAJI wa Nottingham Forest kutoka Korea Kusini, Hwang Ui-jo mwenye umri wa miaka 31, amekubali masharti ya kukaa kwa mkopo katika klabu ya Uturuki ya Alanyaspor. **(Sports Digitale)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ETO'O SASA AKATALIWA KUJIUZULU CAMEROON

**Ni baada ya tuhuma za rushwa na upangaji matokeo, CAF, Fifa wachunguza...**

**YAOUNDE, Cameroon**

SAMUEL Eto'o aliwasilisha barua ya kujiuzulu kama rais wa Shirikisho la Soka la Cameroon juzi, lakini alikataliwa na kamati tendaji.

Eto'o, ambaye alishinda tuzo ya mchezaji bora wa Afrika mara nne, amegubikwa na tuhuma za upangaji matokeo na rushwa.

Shirikisho hilo lilisema kamati yake ya utendaji ilikutana katika Mji Mkuu wa Cameroon, Yaounde, Jumatatu kutathmini kiwango cha timu ya taifa kwenye Kombe la Mataifa ya Afrika, na kwamba mkutano huo ulianza kwa Eto'o kujitolea kuachia ngazi huku akiwaalika wajumbe wengine kufanya hivyo kwa nia njema.

„Mwisho wa majadiliano na mashauriano yaliyofuata, wajumbe wa kamati ya utendaji waliamua kudumisha majukumu yao ya sasa na hivyo kukataa kwa kauli moja kujiuzulu kwa rais na hivyo kufanya upya imani yao kwake ya kuendelea na moyo ule ule wa ujenzi na maendeleo ya soka la Cameroon," taarifa ya shirikisho hilo ilisema.

Shirikisho halikutaja katika taarifa ya maamuzi mengine yoyote yaliyochukuliwa au hitimisho lililotolewa.

Mustakabali wa kocha wa Cameroon, Rigobert Song haukuwa na uhakika baada ya kampeni ya kusikitisha ya Kombe la Afrika.

Eto'o, ambaye alisherehekea na timu hiyo baada ya ushindi wake wa kishindo dhidi ya Gambia katika mchezo wao wa mwisho wa kundi, amekumbwa na tuhuma za rushwa.

Wiki iliyopita, gazeti la The Athletic liliripoti kwamba liliona ujumbe wa WhatsApp, barua pepe, barua na rekodi za sauti ambazo zinadaiwa kuunga mkono shutuma mbalimbali, zikiwamo kupanga mechi, matumizi mabaya ya madaraka, vitisho vya kimwili, kuchochea vurugu na kueneza habari za uongo nchini Cameroon.

Faili la taarifa hiyo limetumwa kwa kamati ya maadili ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), na kwamba inachunguzwa pia na Shirikisho la Soka Afrika, Caf.

CAF tayari ilikuwa inachunguza kile ilichosema ni tuhuma „zito" kutoka kwa „wadau kadhaa wa soka wa Cameroon" dhidi ya Eto'o.

Ilibainisha kuwa nyota huyo wa zamani wa Barcelona na Inter Milan „alidhaniwa kuwa hana hatia hadi chombo kinachofaa cha mahakama kitakapohitimisha vinginevyo."

Soka la Cameroon lilikuwa na matatizo mengi siku za nyuma, kabla ya Eto'o kuchaguliwa kuwa rais, ligi ya taifa ilikuwa imechafuliwa na kuingiliwa na serikali, madai ya ufisadi na kuvunjwa kwa ahadi kutoka kwa viongozi wa soka.

Eto'o aliichezea Cameroon katika fainali nne za Kombe la Dunia kati ya 1998 na 2014.



# FAINALI KOMBE LA DUNIA 2026 KUZINDULIWA UWANJA 'GOLI LA MKONO WA MUNGU'

**NYON, Uswisi**

SHIRIKISHO la Soka la Kimataifa, Fifa, limetangaza tarehe ya ufunguzi Kombe la Dunia la mwaka 2026.

Rais wa Fifa, Gianni Infantino, ametangaza kuwa ufunguzi wa fainali hizo utafanyika Juni 11, 2026.

Infantino ametaja uwanja utakaofungua michezo hiyo kuwa ni wa Azteca uliopo nchini Mexico itakapofanyika sherehe na mechi ya kwanza ya ufunguzi.

Uwanja wa Azteca unaobeba mashabiki 83, ndipo ilipofanyika fainali ya Kombe la Dunia mwaka 1986 kati ya Argentina na England ambapo Diego Maradona alifunga goli maarufu la Mkono wa Mungu 'Hand of God'.

Michuano hiyo itafanyika katika miji 16 iliyopo katika nchi tatu za Canada, Mexico na Marekani.

Fainali hizo zitahitimishwa Julai 19, 2026 katika Uwanja wa MetLife, New Jersey uliopo New York nchini Marekani.

# Foden: Sasa nafurahia nafasi ninayocheza

**LONDON, England**

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Phil Foden, amesema anafurahia nafasi anayocheza sasa chini ya Pep Guardiola baada ya kupachika mabao matatu 'hat-trick' dhidi ya Brentford, juzi.


Mabingwa hao wa Ligi Kuu England walitoka nyuma na kuwafunga ,Nyuki' hao na mchezaji huyo wa Kimataifa wa England alikuwa katika kiwango bora kabisa huko London Magharibi.

Huku jeraha la hapo awali la Kevin De Bruyne likimpa Foden fursa ya kuingia kwenye nafasi yake, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, amefanya zaidi na kuibeba timu yake wakati Mbelgiji huyo hayupo.

Ameendelea kucheza katikati tangu kurejea kwa nahodha wake na anakiri anahisi ni nafasi yake bora zaidi.

Foden alisema: „Nimefurahishwa sana na uchezaji wangu na ninacheza dakika nyingi ndani, mahali ninapotaka kuwa, na nimefurahishwa na jinsi ninavyocheza.

„Ninacheza kiwango bora zaidi ambacho nimekuwa nacho katika jezi ya



City mara kwa mara kwa muda mrefu na huenda hilo likaendelea na nitaendelea kufanya kazi kwa bidii kwenye uwanja wa mazoezi.

„Mimi ni mtu ambaye hubadilika na kucheza nafasi nyingi inapohitajika. Najua nitafanya hivyo nikiwa na Manchester City na lazima niwe tayari.

„Ninafurahia kucheza katikati na hapo ndipo ninapojiona. Natumai naweza kupata muda zaidi wa kucheza huko.

„Nilichojiwekea ni kujaribu kuboresha takwimu za mwaka jana na kujaribu tu kuboresha kila mwaka, malengo zaidi na kusaidia zaidi.

„Nahitaji kuendelea na kuonesha kiwango hiki cha uchezaji mara nyingi zaidi. Sifungi mabao mengi ya vichwa kwa hiyo nimefurahishwa na hilo."

Kocha Guardiola alifurahishwa na mchango wa Foden kwenye Uwanja wa Gtech Community na akataja nambari yake ya 47 kama „ya kushangaza".

Aliongeza: „Siku zote alikuwa na jicho la kufunga. Tayari ana mechi 250 na amekuwa na matokeo mazuri katika kufunga mabao msimu huu. Ni mzuri sana. Namba yake ni nzuri sana."

City sasa wako nyuma kwa pointi mbili dhidi ya vinara wa ligi Liverpool, lakini watakwea kileleni iwapo watashinda mchezo wao mkononi baadaye mwezi huu.

# Barca bado haijatafuta kocha mpya

**BARCELONA, Hispania**

MKURUGENZI wa Michezo wa Barcelona, Deco, amesisitiza kuwa klabu hiyo bado haijafanya mazungumzo na watu wanaoweza kuchukua nafasi ya kocha anayeondoka, Xavi.

Xavi ataondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu, akisema uchovu wa kiakili kama sababu ya kuondoka kwake, na uvumi umeenea kuhusu nani wa kuchukua mikoba yake pale Katalunya.

Jurgen Klopp, ambaye ataondoka Liverpool katika majira ya joto, ni miongoni mwa watu wanaolengwa sana, lakini Deco alikataa kuhusishwa na uvumi huo na akafichua mchakato wa kupata kocha mpya bado haujaanza.

„Klopp ni kocha mzuri, lakini sidhani kama huu ni wakati wa kuzungumza juu yake," alisema akiliambia gazeti la La Vanguardia.

„Kocha mpya atataka kufanya mabadiliko, lakini kwanza itabidi tumweleze mradi na mawazo. Kuna chaguzi nyingi."

Miongoni mwa wanaotajwa ni Thiago Motta, ambaye amevutia sana kule Bologna na Rafa Marquez, ambaye hivi karibuni alikiri hataweza kukataa ofa ya kupandishwa daraja katika klabu hiyo.

„Sifuatilii sana kazi ya Motta kwa sababu hayuko katika timu za Italia ambazo nazifuatilia," alikiri Deco.

„Ninafanya na Marquez, kwa sababu yuko hapa. Ni kocha mchanga ambaye anakua katika hali ya matatizo. Kuwa hapa kutamfanya kuwa kocha bora."

Deco aliendelea: „Kwa sasa, hatujazungumza na kocha yeyote. Bado tunashughulikia kuondoka kwa Xavi.

„Kocha mpya anatakiwa kufuata mstari wa kazi. Kamwe hatutakuwa timu ambayo haitaki kucheza vizuri, ambayo haitaki kuwa na mpira. Kuanzia kwenye wazo hilo, kila kocha ana sifa zake, lakini yeyote anayekuja lazima awe na njaa ya kufanya mambo makubwa."



HABARI MICHEZO

# GAMONDI AKIRI LIGI KUU NGUMU

**Oliver Albert na Saada Akida**

LICHA ya kukiri Ligi Kuu Bara imekuwa ngumu baada ya kushuhudia kikosi chake kikipata ushindi wa tabu na finyu wa bao 1-0 dhidi ya Dodoma Jiji FC juzi, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema bado ana matumaini makubwa kwa timu yake kuweza kutetea ubingwa wa ligi hiyo msimu huu.

Aidha, Gamondi amewasifu wachezaji wake kwa kupambana na kuweza pointi tatu zilizowaweka kileleni huku akiwataka kujituma zaidi katika michezo ijao kwani mbio za ubingwa zimekuwa kali.

Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Azam Complex. Dar es Salaam juzi usiku, Yanga ilibidi kusubiri hadi dakika ya 86 kupata ushindi wa bao1-0 dhidi ya Dodoma Jiji uliowapeleka kileleni kwenye msimamo wa ligi wakifikisha pointi 34 mbele ya Azam iliyoshuka hadi nafasi ya pili ikiwa na pointi 31 wakati Simba ambayo jana jioni ilikuwa ikicheza na Tabora United ilikuwa nafasi ya tatu ikiwa na alama 26.

Gamondi aliwaambia waandishi wetu kuwa pamoja na kwamba Dodoma Jiji walikuwa wakipoteza muda, lakini wachezaji wake walijua jinsi gani ya kucheza nao jambo lililowasaidia kupata ushindi katika mchezo huo.

„Niwapongeze wachezaji wangu, walicheza vizuri muda mwingi wa mchezo licha ya kwamba wapinzani walikuwa wakipoteza muda sana mara kwa mara.

„Tulitengeneza nafasi nyingi, lakini mwisho tukapata goli moja hilo ndilo la muhimu kwani kitu cha muhimu tulichohitaji ni kutumbukiza mpira nyavuni.

„Licha ya kwamba bado tumeendelea kuwakosa baadhi ya wachezaji, lakini hilo halisumbui kwani kila mara tumekuwa tukizidi kuwa bora, mchezo huu tumecheza vizuri kuliko ule uliopita (dhidi ya Kagera Sugar), hivyo naamini tutazidi kuwa vizuri kwa michezo mingine ijayo,@ alisema Gamondi.

Yanga inawakosa baadhi ya nyota wake wa kikosi cha kwanza hususan Djigui Diarra na Stephen Aziz Ki, ambao walikuwa wakizitumikia timu zao za taifa (Mali na Burkina Fasa) kwenye michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon) 2023 nchini Ivory Coast.

Kocha huyo raia wa Argentina, alisema mbio za ubingwa zimekuwa kali, lakini wanakwenda kidogo kidogo na kwa uangalifu kuhakikisha kuwa hawaharibu malengo yao.

Bao pekee la ushindi lilifungwa na Mudathir Yahya dakika ya 86 akitumia vema pasi ya Dickson Kibabage, wote wawili walitokea benchi kipindj cha pili na kuzima ndoto za Dodoma Jiji waliokuwa wanakaribia kupata pointi moja ya ugenini.

Kiungo Mudathir ambaye alifunga bao pekee la ushindi, alisema alipewa maelekezo na kocha wake (Gamondi) kuwa anatakiwa kupanda na kushuka na kuwa makini na nafasi zinazopatikana kuzitumia vema kupata bao.

"Nilitamani sana kufunga hii mechi, kocha alinipa maelekezo na nimeenda kuyafanyia kazi kwa kile nilichoambiwa kwa kufanya majukumu yangu ya kuhakikisha naenda kushambulia na kuhakikisha nazuia, tulifanikiwa na kupata bao la ushindi kwa kuvuna pointi tatu muhimu," alisema Mudathiri.

# Muuza matunda ashinda mil. 10/- magifti dabodabo

**Na Mwandishi Wetu**

MFANYABIASHARA wa matunda na mkazi wa jijini Tanga, Salim Ndaro, ametangazwa kuwa mshindi wa promosheni ya Magifti Dabodabo inayoendeshwa na Kampuni ya Tigo na kukabidhiwa Sh. milioni 10.

Akizungumza nyumbani kwake juzi wakati akikabidhiwa hundi ya fedha hizo, Ndaro alisema fedha alizopata zitamsaidia kukarabati nyumba yake na nyingine kuongeza mtaji wake wa matunda.

"Nashukuru sana kwa kweli kwa ushindi huu, nina furaha sana, ni ngumu kwangu kuzipata fedha nyingi hivi kwa wakati mmoja, zitanisaidia sana," alisema Ndaro.

Akizungumzia namna alivyoshinda, mshindi huyo alisema alikuwa akifanya miamala ya kununua muda wa maongezi mara kwa mara, na kisha alijikuta akipigiwa simu na wafanyakazi wa Tigo wakimtaarifu ameibuka mshindi wa shilingi milioni 10.



Mashindi wa Sh. milioni 10 kwenye Promosheni ya Magifti Dabodabo, Salim Ndaro (kushoto), akizungumza jana na waandishi wa habari mbele ya nyumba yake jijini Tanga baada ya kukabidhiwa mfano wa hundi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

"Sikuamini kwa kweli mpaka waliposema wanakuja nyumbani kwangu kunikabidhi hundi, nawashauri wateja wengine washiriki kwa kufanya miamala mingi," alisema Ndaro.

Kwa upande wa Meneja Mauzo wa Tigo Kanda ya Pwani, Abdul Ally, alisema kwa sasa imebaki droo moja ambayo ni kubwa kwa ajili ya kumtangaza mshindi wa gari jipya atakalokabidhiwa.

"Mshindi huyu wa gari atakayepatikana kwenye droo yetu ya mwisho atapata fursa ya kumchagua mtu mmoja ampendaye ambaye naye atapewa zawadi ya gari jipya kama ambavyo promosheni hii inasema magifti dabodabo," alisema Ally.

Promosheni hiyo ilizinduliwa rasmi Novemba mwaka jana na inatarajiwa kukamilika mwezi huu kwa kutoa zawadi ya gari na fedha shilingi milioni 30 kwa washindi wa droo hiyo.

## Nigeria vs Afrika Kusini, Ivory Coast vs DRC leo

INATOKA UK. 24

tika hatua ya makundi, kabla ya kuwatoa mabingwa Senegal kwa mikwaju ya penalti na kisha kuwabana Mali 2-1 baada ya muda wa ziada.

Ivory Coast inatazamiwa kuwakosa Oumar Diakite na Odilon Kossounou baada ya wawili hao kutolewa nje kwa kadi nyekundu kwenye mchezo uliopita.

Kumpoteza Diakite kutamfadhaisha zaidi kocha wa muda, Emerse Fae, hii ni baada ya mchezaji huyo kupewa kadi ya pili ya njano kwa kuvua shati lake akisherehekea bao lake la ushindi katika muda wa ziada.

Sebastien Haller anapigania nafasi ya kuanza mbele baada ya kupona jeraha la kifundo cha mguu, wakati Willy Boly anaweza kuingia kwenye safu ya ulinzi kuchukua nafasi ya Kossounou aliyefungiwa.

**DR CONGO**

DR Congo walitoka sare katika michezo yao yote mitatu ya makundi, kabla ya kushinda kwa mikwaju ya penalti dhidi ya Misri na kufuzu robo fainali kwa ushindi wa 3-1 dhidi ya Guinea.

Kocha Mkuu wa DR Congo, Sebastien Desabre, hana wasiwasi wowote baada ya ushindi wa mabao 3-1 wa ‚Chui' hao dhidi ya Guinea katika robo fainali.

**TAKWIMU**

Mara ya mwisho timu hizi zilikutana Oktoba 2019, Ivory Coast ikitoka na ushindi wa 3-1 katika mchezo wa kirafiki Uwanja wa Licorne mjini Amiens, Ufaransa.

Timu zote mbili zimehusika katika mechi moja pekee ambapo kulikuwa na zaidi ya mabao mawili yaliyofungwa katika muda wa kawaida kwenye Kombe hili la Mataifa ya Afrika.

# Kouablan 'mabao' aanza kazi Simba, Tabora United ikifa

INATOKA UK. 24

Sadio Kanoute aliongeza bao la pili dakika ya 38 kwa kichwa, baada ya kuunganisha krosi iliyopigwa na Shomari Kapombe.

Ilikuwa kazi nzuri ya Kibu ambaye aliambaa na mpira wingi ya kushoto na kulazimisha beki Said Mbatty kuuokoa na ilionekana kama unakwenda kutoka kona au wa kurushwa, lakini ukawahiwa na Kapombe aliyeurudisha ndani na kusababisha bao la pili.

Lilikuwa ni bao la pili kwa Kanoute kwenye Ligi Kuu, la kwanza akilifunga pia kwa kichwa, Desemba 15, mwaka jana, Simba ikiifunga Kagera Sugar mabao 3-0, Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Mabao hayo ya Jobe na Kanoute yanaifanya Simba kufikisha mabao matano yaliyofungwa kwa vichwa kati ya 28 iliyonayo mpaka sasa kwenye ligi. Kanoute ana mabao mawili, Jobe, Fabrice Ngoma na Kibu moja moja.

Beki wa kati Fondoh Che Malone alifunga bao lake la kwanza tangu ajiunge na timu hiyo mwanzoni mwa msimu, akipata pande safi kutoka kwa Clatous Chama.

Bao hilo alililofunga dakika ya 59, lilitokana na mpira wa kona wa Saido ambao ulimponyoka John Boble, ukaokolewa kizembe na mabeki wa timu hiyo, ukatua miguuni mwa Chama ambaye alimsogezea mfungaji.

Kouablan alipigilia msumari wa mwisho kwenye jeneza la Tabora United dakika nne kabla ya mechi kumalizika, baada ya kumzunguka Erick Ogutu na kupiga shuti dhaifu lililomhadaa kipa Noble kabla ya kujaa wavuni.

Simba imeendeleza ushindi wa asilimia 100 ikicheza ugenini, ambapo katika mechi zote nne imeshinda zote kwa kuifunga Mtibwa Sugar 4-2, Mashujaa FC 1-0, Singida Fountain Gate mabao 2-1, Prisons mabao 3-1, kabla ya mechi ya jana.

Simba ilianza mechi kwa kasi na dakika ya kwanza tu, Kibu Denis alimjaribu kipa John Noble kwa shuti la mguu wa kushoto akiwa nje kidogo ya eneo la hatari, lakini ukatoka nje.

Chama naye karibia kuiandikia timu yake bao dakika ya 11, lakini kama ilivyokuwa kwa shuti la Kibu, mpira ukatoka na dakika nne baadaye Saido Ntibazonkiza akaungana na wenzake kupiga shuti la tatu nje.

Kennedy Juma, nusura aiandikie Simba bao dakika ya 17, aliporuka juu kuunganisha mpira wa kona iliyopigwa na Saido.

Kama Simba ingekuwa makini kipindi cha kwanza ingeweza kuvuna mabao mengi, lakini wachezaji wake walikosa mabao mara kadhaa, Chama akikosa mawili akiwa ana kwa ana na kipa Noble, baada ya kuwalamba chenga mabeki wa Tabora United, huku Saido na Jobe nao wakijichanganya wenyewe.

Ni kipindi ambacho Tabora United haikufanya shambulizi lolote la maana kwenye lango la Simba lililokuwa chini ya Ayob Lakred.

Kipindi cha pili baada ya mabadiliko Tabora United ilibadilika na kucheza mchezo wa kasi, lakini haikuweza kufanya chochote mbele ya Simba.

Kwa matokeo hayo, Simba sasa imefikisha pointi 29, ikicheza mechi 12, lakini ikiwa bado kwenye nafasi ya tatu ya msimamo wa ligi nyuma ya Azam FC (pointi 31) na vinara Yanga wenye alama 34, huku Tabora United ikiwa nafasi ya 12, pointi 15, baada ya kucheza michezo 14.

Michezo
Jumatano Februari 7, 2024
Nipashe

Eto'o sasa akataliwa kujiuzulu Cameroon UKURASA 21






# NIGERIA VS AFRIKA KUSINI, IVORY COAST VS DRC LEO

## ●●●Nani kutinga fainali? Takwimu zatoa nafasi kwa...

**ABIDJAN, Ivory Coast**

NIGERIA na Afrika Kusini zitamenyana kwenye nusu fainali ya kwanza ya michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon), kule mjini Bouake saa mbili usiku leo Jumatano, huku Ivory Coast ikiiva Jamhuari ya Congo (DRC) kwenye nusu fainali ya pili majira ya saa tano usiku katika Uwanja wa Olympique Alassane Ouattara jijini Abidjan, wakiwania kutinga fainali itakayopigwa Jumapili.

Nigeria imefungwa bao moja pekee kuelekea nusu fainali, huku Afrika Kusini ikiruhusu mawili na hakuna taifa lililofungwa tangu mchezo wao wa ufunguzi wa hatua ya makundi.

**NIGERIA**

Ahmed Musa na Kelechi Iheanacho bado wanafuatiliwa hali zao kiafya, lakini wote wanatatarajiwa kuwa kwenye benchi la Nigeria.

Kocha Jose Peseiro anatazamiwa kutaja kikosi cha kwanza akitumia mfumo wa 3-4-2-1 kwa mechi ya tatu mfululizo.

**AFRIKA KUSINI**

Kocha wa Bafana Bafana, Hugo Broos hana wasiwasi mpya wa jeraha hivyo pia anatazamiwa kubaki na wachezaji wale wale - katika mfumo wao wa 4-2-3-1 - walioichezea Cape Verde.

**TAKWIMU**

Mechi tano za Nigeria nchini Ivory Coast zimezalisha mabao saba, huku mchezaji Ademola Lookman akifunga mabao matatu ya Super Eagles katika raundi mbili za mtoano.

Afrika Kusini imeshindwa kufumania nyavu katika mechi tatu kati ya tano kwenye michuano hiyo.

Afrika Kusini mara ya mwisho ilifungwa katika mchezo wao wa kwanza wa makundi.

**UTABIRI**

Afrika Kusini wameshinda michezo miwili pekee kati ya mitano hadi sasa, huku Nigeria wakiwa hawajafunga zaidi ya mabao mawili katika mchezo mmoja.

**IVORY COAST**

Ni mwenyeji wa mashindano haya na anawania kulitwaa taji hilo kwa mara ya tatu katika historia yake.

Tembo hao mara ya mwisho walileba taji hilo mwaka 2015, wakati DR Congo wamelitwaa taji hilo mara mbili, lakini ushindi wao wa mwisho ulikuja mwaka 1974.

Ivory Coast ilishindwa kutamba ka

INAENDELEA UK. 23

## Kouablan 'mabao' aanza kazi Simba, Tabora United ikifa

**Na Adam Fungamwango**

MASTRAIKA wawili waliosajiliwa kipindi cha uhamisho wa dirisha dogo Januari mwaka huu, Pa Omar Jobe na Freddy Michael Kouablan, kila mmoja jana alifunga bao, wakiiongoza Simba kupata ushindi mnono wa mabao 4-0 dhidi ya timu ngumu ya Tabora United, mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara ikipigwa, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora.

Jobe raia wa Gambia na Freddy, wamefunga mabao yao ya kwanza kwenye Ligi Kuu wakicheza mechi ya pili, baada ya ile ya kwanza dhidi ya Mashujaa kushindwa kufanya hivyo.

Ilikuwa ni dakika ya 19, Jobe, alipoandika bao la kwanza, akiruka juu kuunganisha mpira wa faulo iliyopigwa na Chama, baada ya yeye mwenyewe kuangushwa nje kidogo ya eneo la hatari na Andy Bikoko.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >